**RAIS** mstaafu Ellen Sirleaf wa Liberia ampa neno Samia

UKURASA 3



**WATU** 14 wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kuua kwa kukusudia

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Ijumaa Machi 26, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580531

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710


# CHATO YAZIZIMA

**MAELFU** wajitokeza kuaga mwili wa JPM, shughuli zasimama, bei za bidhaa zapanda...

*Endelea Ukurasa 2*



Maofisa wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakitoa heshima za mwisho kwa mwili wa aliyekuwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Magufuli, Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: IKULU**

## Baba asimulia vifo vya watu sita wa familia moja

UKURASA 2



Majeneza yenye miili ya wanafamilia waliopoteza maisha wakati wa kumuaga Hayati Dk. John Magufuli katika Uwanja wa Uhuru, wakati wa ibada ya kuwaaga katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kimara Korogwe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**MICHEZO** SIMBA YABADILISHA GIA KUIVAA AS VITA UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Chato yazizima kuaga mwili wa JPM

**Na Richard Makore,** CHATO

MJI wa Chato jana ulitandwa na simanzi na vilio wakati wananchi walipouaga mwili wa Hayati Rais John Magufuli, huku shughuli mbalimbali za kiuchumi zikisitishwa kwa muda.

Wakazi wa Chato na maeneo jirani waliofika kwenye Uwanja wa Magufuli, walipata fursa ya kuuaga mwili wa mpendwa wao huyo, wakianza kuingia uwanjani mapema asubuhi.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Mazishi Kitaifa, Hemed Seleman Abdulla, aliongoza wananchi hao kuuaga mwili huo uliofikishwa Chato juzi jioni.

Katika kipindi chote cha kuaga mwili huo uwanjani, wananchi walioshiriki, walionekana kukaa kimya kwenye viti vyao, baadhi wakilia kutokana na kumpoteza kiongozi huyo aliyejizolea umaarufu mkubwa duniani kutokana na misimamo yake.

Akizungumza na waombolezaji hao, Abdulla alimwelezea Hayati Magufuli kama kiongozi aliyekuwa makini na asiyekuwa na ubaguzi wa kabila wala dini.

Alisema Hayati Magufuli amemaliza kazi yake duniani na kuwaomba Watanzania kuzidi kumwombea apokewe na Mwenyezi Mungu.

Mji wa Chato kuanzia juzi jioni ulipoingia mwili wa Hayati Magufuli, ulionekana kuzidiwa na idadi ya watu huku wageni wengine wakikodisha nyumba za watu binafsi ili kupata pa kulala.

Wageni wengine baada ya kukosa vyumba katika nyumba za kulala wageni, waliamua kwenda kulala mjini Geita, Buseresere na Katoro.

Baadhi ya wafanyabiashara walifunga maduka yao wakati wa kuaga mwili huo, huku migahawa iliendelea kuwa wazi na ingawa vyakula vilipungua katika sehemu mbalimbali na hivyo wateja kulazimika kusubiri.

Kutokana na wingi huo wa wageni, bei ya vyakula hususani nyama ya kuku na mbuzi, ilipanda. Katika baadhi ya migahawa, nyama ya mbuzi iliuzwa kwa Sh. 16,000 badala ya Sh. 8,000 kwa kilo moja ilivyokuwa awali.

Vilevile, nyama ya kuku mzima iliuzwa kati ya Sh. 25,000 na 30,000, huku ikionekana kupungua jana mchana baada ya baadhi ya wananchi kumaliza kuaga mwili na kuingia mtaani.

Kwenye maeneo na kumbi za starehe, kulionekana kufurika watu kuanzia juzi jioni baada ya mwili wa Hayati Magufuli kufikishwa mjini Chato ukitokea mkoani Mwanza.

Mbali na Abdulla, viongozi wengine walioshiriki kuuaga mwili wa Hayati Magufuli mjini Chato ni pamoja na Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, makatibu wakuu wa wizara, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama na familia ya marehemu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na serikali, leo ndiyo siku ya maziko ambayo yatafanyika katika makaburi ya familia yaliyoko Kijiji cha Mlimani wilayani Chato mkoani Geita.

Dk. Magufuli, Rais wa Tano wa Tanzania, alifariki dunia majira ya saa 12 jioni Machi 17, mwaka huu, kutokana na ugonjwa wa moyo na kifo chake kutangazwa siku hiyo majira ya saa tano usiku na aliyekuwa Makamu wake na sasa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Wakati mwili wa Hayati Magufuli ukiwasili nyumbani kwake wilayani Chato juzi, kulikuwa na umati mkubwa wa wananchi waliotanda barabarani huku vilio na simanzi vikitawala.

Mwili ulifikishwa Chato majira ya saa 12 jioni huku msafara wake ukisindikizwa na chopa mbili za kijeshi. Wananchi walibeba matawi ya miti, mabango na kutandika kanga barabarani.



Mtoto wa Hayati Dk. John Magufuli, Joseph Magufuli, akitoa heshima zake za mwisho kwa mwili wa baba yake, katika Uwanja wa Magufuli, Chato mkoani Geita jana . **PICHA: IKULU**

## Baba asimulia ya kutisha vifo vya watu sita wa familia moja

**Na Waandishi Wetu**

DENIS Mtuwa, baba aliyepoteza mke, watoto wake wawili pamoja na watoto wa ndugu zake wawili wakati wa kuaga mwili wa Rais John Magufuli mkoani Dar es Salaam Jumapili, amesimulia alivyopata taarifa na miili ya ndugu zake hao.

Mbali na ndugu hao watano wa familia moja kufariki dunia siku moja, familia hiyo pia ilipoteza msichana wa kazi katika tukio hilo hilo.

Akisimulia mkasa huo uliosababisha kupoteza mke na watoto, Mtuwa aliwaambia waombolezaji kanisani KKKT Kimara mkoani Dar es Salaam jana kuwa, alipigiwa simu na mwandishi wa habari wa TBC ili akachukue simu na vitu vingine vya mkewe.

"Ilikuwa kimya mpaka saa saba mchana nilipopigiwa simu na mwandishi wa habari wa TBC, akasema ameokota simu ya mke wangu, ameanguka uwanjani.

"Mimi nilijua labda tu amepata hofu baada ya kuaga mwili. Basi, yule mwandishi akaniambia njoo sasa hivi hapa Taifa (Uwanja wa Taifa karibu na Uwanja wa Uhuru kulikokuwa na shughuli ya kuaga mwili wa Rais Magufuli). Uje uchukue simu na pochi yake na kadi za benki na vitambulisho vya kazini," alisema.

Mtuwa alisimulia kuwa baada ya kufika Uwanja wa Uhuru na kuwakosa ndugu zake hao, alielekezwa kwenda Hospitali ya Temeke ili kuona iwapo miongoni mwa majeruhi walikuwa ndugu zake, lakini alishangaa baada ya kuwakuta watano kati ya sita wakiwa mochwari.

Alisema awali watoto walimwomba mama yao kwenda kuuaga mwili wa Hayati Magufuli kwenye Uwanja wa Uhuru kwa kuwa walikuwa wakimpenda kiongozi huyo wa nchi.

Kwa mujibu wa Mtuwa, siku ya tukio mke wake na watoto hao waliamka mapema, wakajiandaa kwa ajili ya shughuli hiyo na saa 12 kasoro asubuhi waliondoka nyumbani kwa gari la familia na kufika uwanjani saa moja na nusu asubuhi.

Alisema kuwa baada ya kufika uwanjani, walipiga picha na kuwatumia nyumbani kuwa tayari wameshafika wakiwa wote sita, yaani mkewe, watoto wake wawili, watoto wawili wa kaka zake wawili pamoja na dada wa kazi, lakini baadaye saa 7 mchana alipigiwa simu na mwandishi wa habari na kupewa taarifa za kutakiwa uwanjani.

**USHAURI KWA SERIKALI**

Mtuwa alisema mkewe Susan alikuwa mhasibu huku akiiomba serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuingia na kutoka kwenye matukio makubwa kama hilo la kuaga mwili wa Hayati Rais Magufuli.

"Kwenye matukio ya kitaifa, kuwe na uratibu wa kuwakinga watoto na watu wenye ulemavu kuingia na kutoka uwanjani kwenye matukio kama hayo," alisema mgane huyo.

Watoto wake waliofariki dunia ni Natalia na Nathaniel na wengine wawili ambao ni wa ndugu zake; Michele na Christian pamoja na msichana wa kazi za nyumbani ambaye taratibu za maziko yake zinatarajiwa kujulikana baada ya kikao na ndugu zake kutoka mkoani Njombe.

Miili ya watu hao watano iliyoagwa jana kanisani, ilizikwa kwenye eneo la familia Kimara wilayani Ubungo baada ya kupewa kibali na serikali.

**VILIO KANISANI**

Huzuni, simanzi na vilio vilitawala jana baada ya mamia ya waombolezaji kushuhudia majeneza matano yenye miili ya wanafamilia hao watano yakiingizwa kwenye Kanisa la Kiinjili la Kirutheri Tanzania (KKKT) Kimara wilayani Ubungo jana majira ya saa sita mchana.

Mchungaji Wilbroad Matsai, akihubiri katika ibada hiyo, alisema ni tukio la kusikitisha zaidi katika maisha ya miaka 20 ya utumishi wake na kwa mara ya kwanza kwake kuongoza ibada kukiwa na majeneza matano mbele yake.

"Mimi ni baba yao wa kiroho wote hawa sita, ninajihisi nami ninahitaji faraja. Kwa hakika, nimeumia! Siwezi kuwazuia ndugu kulia. Tuwaombee kwa Mungu wa rehema awaondolee uchungu na maumivu ya kuondokewa na ndugu zao, maana yeye ndiyo anamiliki uzima na mauti," alisema.

Aliwaonya watu ambao wamekuwa wakizungumza maneno yasiyostahili kuhusu vifo, akibainisha kuwa ni vyema kumwachia Mungu kwa kuwa alikuwa na uwezo wa kuzuia watu hao wasife kwa aina hiyo ya kifo.

Aliwashukuru Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, na Mbunge wa Kibamba, Issa Mtemvu, waliofika kwenye ibada hiyo.

Siku hiyo, ambayo ilikuwa ya pili na ya mwisho kwa wakazi wa Dar es Salaam na mikoa jirani kuaga mwili wa Hayati Rais Magufuli, maelfu ya wananchi walifurika uwanjani kutoa heshima za mwisho kwa kiongozi huyo, hali iliyosababisha vifo na majeruhi baada ya watu kukanyagana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Aminieli Eligaisha, Machi 21, hospitali hiyo ilipokea maiti na majeruhi kutokana na tukio hilo.

***Imeandikwa na Beatrice Moses na Enock Charles**

## HABARI KITAIFA

# Rais mstaafu Liberia ampa neno Samia

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS mstaafu wa Liberia, Ellen Johnson Sirleaf, amesema Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ategemee upweke kutokana na kuwa mwanamke wa kwanza Afrika Mashariki kushika nafasi ya juu ya uongozi.

Aliyasema hayo jana alipofanyiwa mahojiano na BBC, ambapo alisema Samia kushika nafasi hiyo ni jambo la kufurahisha na ameingia akiwa ameinuliwa kutoka nafasi aliyokuwa anahudumia ambayo si kubwa kuliko aliyonayo sasa.

Alisema wanawake wote Afrika na hata zaidi wamefurahi kwa kuwa Afrika ina rais mwanamke tena, ingawa ni wachache, lakini pia inaweza kuwa safari ya upweke kwake.

Aliongeza kuwa kutokana na hilo, huwezi kujiunga katika makundi maalumu ili kujadiliana masuala kadhaa na hata hiyo unakuta unatazamwa na wanaume katika mikutano kama mtu aliyetumia nguvu kuingia katika eneo lao.

"Aidha, hiyo inaweza kumfanya asipate aina ya urafiki wanaopata wanaume, lakini kuwa wanawake wengi hupendelea kukabiliana na mambo kama hayo yanapo watokea."

Alisema wanawake wanapenda kujifunza na kuendelea na mambo yao ya kila siku ikiwamo na kuchukua majukumu yao ya uongozi na kuyatekeleza.

Pia alieleza kuwa Afrika haijafikia malengo kulingana na matarajio katika kuwawezesha wanawake kuwa viongozi na kwamba walitarajia kipitia juhudi zilizofanywa kufikia sasa wangefikia mafanikio makubwa.

"Juhudi za kuwawezesha wanawake zimepungua katika miaka ya hivi karibuni, ambapo tumeona kurudi nyuma kwa hatua zilizopigwa katika maendeleo na kasi ya kusonga mbele imepungua sana," alisema.

Sambamba na hilo wanafikia kwamba huko ni kurudi nyuma kwa upande wa wale wanaodhani kwamba wanawake walikuwa wakisonga mbele kwa kasi ya hali ya juu katika kuhakikisha wanafanikiwa.

# ...Askofu asema ana imani naye

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Mara, George Okoth, amesema ana matumaini makubwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan anaweza kuiongoza nchi kama alivyokuwa Hayati Dk. John Magufuli.

Kutokana na imani hiyo, amewataka wananchi wanaoendekeza mfumo dume kuacha tabia hiyo kwa kuwa kiongozi yoyote huwekwa na Mwenyezi Mungu.

Askofu Okoth aliyasema hayo juzi na mwandishi wa habari hii baada kumalizika kwa kikao cha Bodi ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhemba. Baadhi ya wajumbe wa bodi, walimu na wanafunzi walielezea kuguswa na kifo cha Rais Magufuli kwamba alikuwa bado anahitajika na taifa.

Okoth alisema kanisa linafarijika kuwa katika hotuba yake, Rais Samia aliwapa moyo kwa kusema kwamba ndiye Rais na ataweza na nchi itakuwa salama ingawa yeye kijinsia ni mwanamke.

Pia alisema wanaume ambao wamezoea mfumo dume kwamba wanawake hawawezi, wajue kwamba dhana hiyo ni potofu na imepitwa na wakati na kwamba wanawake sasa wanaweza.

"Kazi tuliyo nayo sasa Watanzania ni kumwombea Rais Samia kwani yake hawezi, hivyo anahitaji nguvu za Mungu na ushirikiano wa wananchi wote ili kufanikisha azma yake na kusudi la Mungu la kumchagua kuwa Rais wetu.

Alisema jambo la msingi ni wananchi kuelewa kwamba Samia hajajichagua bali Mwenyezi Mungu ndiye aliyemchagua hadi kufikia hapo alipo.

"Wakati huu tunapoendelea kuomboleza, ni vyema wananchi wote tukawa watulivu na kuendelea na maombi huku tukimtegemea Mwenyezi Mungu kama alivyokuwa Hayati Dk. Magufuli alivyokuwa anamtegemea wakati wote na siku zote.

Na sisi tumtangulize Mungu maana sisi ni wapitaji tu katika dunia hii. Tuishi tukijua kuwa sisi ni wasafiri, tutengeneze maisha yetu ya sasa na ya baadaye, na tujue kuwa kila mmoja alipewa talanta ataifanyia nini talanta aliyopewa," alisema.

**Wakati huu tunapoendelea kuomboleza, ni vyema wananchi wote tukawa watulivu na kuendelea na maombi huku tukimtegemea Mwenyezi Mungu kama alivyokuwa Hayati Dk. Magufuli alivyokuwa anamtegemea wakati wote na siku zote**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI,VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI
(OSHA)

SALAMU ZA RAMBIRAMBI




Bodi ya Ushauri (MAB), Menejimenti na Watumishi wote wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), tunaungana na watanzania wote katika kuomboleza kifo cha aliyekuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Tano, Dkt. John Pombe Magufuli, kilichotokea tarehe 17/03/2021.

Tunapenda kutoa pole kwa familia na watanzania wote. Mungu atupe nguvu katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo.

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)
PO Box 519, Dar es Salaam
Nukushi + 255-22-2760552 | Simu + 255-22-2760548
Barua pepe: info@osha.go.tz

Osha_tanzania_official | Occupational Safety And Health Authority | Tanzaniaosha | Osha Tv Online

# Wahukumiwa kunyongwa kuua kwa kukusudia

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, iliyoketi Geita, imewahukumu watu 14 kunyongwa hadi kufa kwa makosa ya mauaji ya kukusudia.

Washtakiwa hao ni Matongo Mathayo, Juma mohamed, Rubeni Kakinda, Shingela Masai, Maswi Nchala, Robert Sita, Thomas Elias, Sanda Kishosha, Revocatus Stephano, Nikolaus Paulo, Juma Msafiri, Pendo Rumwecha, Masumbuko Daudi na Burabo Marejiwa.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Sam Rumanyika, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kuwa washtakiwa hao walitenda makosa ya mauaji ya kukusudia pasipo kuacha shaka.

Rumanyika alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na kwa watu wengine wenye tabia ya kuua watu kwa makusudi.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi tofauti na vielelezo ambavyo vilithibitisha kuwa washtakia hao waliwaua watu wa sehemu mbali mbali kwa makusudi.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na mawakili wa serikali na kwa upande wa utetezi wa washtakiwa, ulikuwa ukiongozwa na mawakili wa kujitegemea.

Alisema washtakiwa wawili ambao ni Matongo Mathayo na Juma Msafiri wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia, Hadija Rwakunyango.

Pia, alisema mashtakiwa Revocatus Stephano amehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia Shukuru Inoseti.

Alisema mshtakiwa Thomas Elias, amehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia, Hoja ngunguhu.

Jaji Rumanyika alisema washtakiwa wanne, Sanda Kishosha, Pendo Rumwecha, Masumbuko Daudi na Burabo Marejiwa, wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia, Tabu Misungwi.

Alisema washtakiwa watatu, Rubeni Kakinda, Mesodi Cherehani na Sadiki Kabale wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia, Kulwa Kaparata.

Aidha, Jaji Rumanyika alisema katika kesi hizo mahakama inaawachia huru watu wanne kwa sababu upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha mashtaka yao.




Askofu mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Iringa, Dk. Owdenburg Mdegella, akitia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais, Dk. John Magufuli katika Ofisi ya CCM Mkoa wa Iringa jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**.

# BAKWATA yampongeza Uhuru Kenyatta

**Na Mwandishi wetu**

BARAZA Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), limempongeza Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, kwa kusimamisha hotuba yake kwa ajili ya kupisha adhana ya swala ya adhuhuri.

Kenyatta alifanya hivyo Machi 22, mwaka huu, wakati akitoa salam za rambirambi katika viwanja vya Jamuhuri, jijini Dodoma wakati wa mazishi ya kitaifa kwa Hayati Rais John Magufuli.

Wakati akitoa salam za taifa la Kenya, adhana ilisikika kutoka msikiti wa Gadaffi ulioko hatua chache kutoka uwanjani humo na alilazimika kusubiri kwa dakika mbili na sekunde 30 kupisha adhana hiyo.

Taarifa iliyotolewa na BAKWATA jana ilisema: "Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), chini ya Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar bin Zubeir Bin Ali Mbwana, linapenda kutoa pongezi kwa rais Kenyatta kwa kusimamisha hotuba yake ili kupisha adhana ya swala ya adhuhuri mjini Dodoma wakati wa kutoa salam za rambirambi za kumuaga aliyekuwa Rais Magufuli. Rais Kenyatta tunakutakia kila laheri katika majukumu yako."

Tangu Rais Uhuru afanye hivyo, pongezi mbalimbali zimemiminika kwenye mitandao ya kijamii, huku waislam nchini Kenya wakitoa taarifa ya pongezi kwa kuheshimu adhana hiyo.

"Kipimo cha uelewa uliopitiliza katika mambo mengi ya kidunia. Sina uhakika kama kuna kiongozi amewahi kufanya hivi. Na sina uhakika kama kuna mwingine angefanya hivi," aliandika mtu anayejiita Baba Watoto.

## Tembo waua wawili Tunduru

**Na Stevie chindiye,**

Tunduru

WATU wawili katika vijiji vya Mpanji katika Kata ya Kidodoma na Kijiji cha Kalulu Kata ya Kalulu wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamekufa baada ya kushambuliwa na tembo.

Taarifa zinaeleza kuwa tukio la kwanza lilitokea Jumanne majira ya usiku baada ya kundi la tembo kuvamia shambani kwa marehemu aliyetambulika kwa jina Sofia Mbemba Ally (56).

Diwani wa kata hiyo, Motta Mbale, alisema Sofia alikanyagwa sehemu za tumbo na kusababisha utumbo wake kutoka nje pamoja na kuvunja mguu wa kushoto.

Mume wa Sofia, Sisi Abdele, alisema mkasa huo ulimkuta mkewe wakati yeye akiwa zamu ya kulala nyumbani kwa mkewe mdogo na kwamba Sofia ameacha watoto saba.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, tukio la pili lilitokea katika mashamba yaliyopo Kitongoji cha Mkasale katika Kijiji cha Mpanji ambapo mwanamume mmoja aliyetambulika kwa jina la Mohamedi Omari Kitemwe (45), kufa majira ya asubuhi juzi.

Baadhi ya mashuhuda walisema Kitemwe alivamiwa na tembo akitoka nyumbani kuelekea shambani baada ya kukutana na kundi la wanyama hao njiani.

Diwani wa Kidodoma, Shambani Nyenje Kuchi, alisema marehemu ameacha mke na watoto watano.

Aidha, wananchi mbalimbali katika maeneo hayo walisema kwa sasa tembo wengi wanazagaa kwenye maeneo ya mashamba ya wakulima na kushambulia mazao.


Ofisa wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Limbega Ally, alikiri kuwapo kwa matukio hayo na kwamba amepeleka vikosi vya askari wa idara hiyo wenye silaha kwa ajili ya kuwafukuza tembo hao na kuwarudisha kwenye maeneo ya hifadhi ili wasiendelee kuleta madhara kwa wananchi.


## TANGAZO

TPA
TANZANIA PORTS AUTHORITY

# MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA)




















# BURIANI

## Dkt. John Pombe Joseph Magufuli

## 1959-2021

**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kwa majonzi makubwa, wanaungana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote kuomboleza kifo cha Rais wa awamu ya Tano, Mhe.Dkt John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi 2021.**

**Daima tutauenzi uchapakazi wake, uzalendo, ujasiri, uadilifu, uwazi na uwajibikaji uliotukuka katika kuendeleza sekta ya Bandari Tanzania.**

**Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. AMINA**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Pumzika Magufuli, umetuachia alama*

**MAZIKO** ya aliyekuwa Rais wa tano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu atazikwa leo nyumbani kwake Chato, mkoani Geita.

Kwa siku zote za maombolezo kuanzia Machi 18 hadi jana hususan shughuli nzima za kuaga mwili wake kuanzia Jumamosi na Jumapili mkoani Dar es Salaam; Jumatatu (Dodoma); Jumanne (Zanzibar), Jumatano (Mwanza) na jana (Chato) kwa wenye macho wameona na bila shaka wamejifunza jinsi ambavyo Watanzania wamempa heshima kubwa kiongozi huyo.

Heshima hiyo imetokana na jambo moja kubwa; la kuwapa utumishi uliotukuka wakushughulikia na kutatua kero za wengi hasa wanyonge pamoja na kubuni kisha kitekeleza miradi yenye lengo la kukuza uchumi wa taifa na kuwaondolea wananchi umaskini.

Sio lengo letu kuyarudiarudia mambo ambayo Hayati Dk. Magufuli amelifanyia taifa letu, kwa kuwa yamezungumzwa sana na wengi, wakiwamo wakuu wa nchi na serikali katika nchi mbalimbali.

Kinachowafanya Watanzania wengi hususan wanyonge wamlilie sana ni kwa jinsi alivyowatetea na kuwa mstari wa mbele kuwatatulia kero zao kwa papo hapo pale walipoziwasilisha kwake.

Kitu kingine kinachochangia ni jinsi alivyoweza kutekeleza mambo mengi na kuyakamilisha kwa muda mfupi wa kipindi cha miaka mitano aliyokuwa madarakani.

Leo anapozikwa, ameacha mengi mazuri ambayo yanapaswa kuwa alama kwetu na vizazi vijavyo, kwa sababu taifa lolote huru haliwezi kupata maendeleo bila viongozi wake kujitoa kama alivyofanya yeye.

Tanzania imejaliwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwa na rasilimali nyingi kama madini, mafuta, gesi, mifugo, wanyamapori, ardhi kubwa na yenye rutuba, misitu, mito, maziwa na bahari, ambazo zinapaswa kuifanya kuwa mfano kwa uchumi mkubwa kama zitatumika vizuri.

Hayati Magufuli alikuwa na maono hayo, huku akieleza kuwa Tanzania kutokana na rasilimali ilizonazo hakuna sababu za kuwa maskini, hivyo kuamua kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha zinalindwa.

Itakumbukwa jinsi alivyosimamia ujenzi wa ukuta kwa lengo la kudhibiti utoroshaji wa madini ya tanzanite huko Mirerani wilayani Simanjiro, Mkoa wa Arusha. Tulishuhudia jinsi alivyodhibiti ujangili wa wanyamapori kama tembo, faru, twiga, kwa kutaja baadhi katika hifadhi na mapori ya akiba.


Vilevile sisi ni mashuhuda wa udhibiti wa uvuvi haramu katika mito, maziwa na bahari. Hakika matunda yake sasa yameanza kuonekana kwa mfano, mauzi ya tanzanite yameongezeka sana; wanyamapori ambao walikuwa katika hatari ya kutoweka wameanza kurejea kwa kasi na samaki wameongezeka, tena ukubwa wao umeongezeka kulinganisha na kabla ya hatua za udhibiti.

Kutokana na alama aliyoiacha, ndio maana Watanzania wengi walitamani kwenda kumzika huko kijijini leo, lakini haikuwezekana kutokana na eneo lenyewe kutototosheleza umati.

Kila binadamu atapitia njia ya kifo, ila Hayati Dk. Magufuli Mungu amemchukua mapema wakati taifa likiendelea kumhitaji sana. Hata hivyo, tunasema tangulia, pumzika Magufuli, umeacha alama, utadumu kwenye mionyo ya wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Maulid Mmbaga

# *Tunampumzisha leo, ila tubaki milele tukiyaenzi aliyotuachia kivitendo*

**WATANZANIA** wamkumbuke aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Dk. John Magufuli, kwa kuyaenzi aliyokuwa anayafanya enzi za uhai na uongozi wake, katika uzalendo na kufanya kazi kwa bidii, kwa manufaa ya taifa zima.

Rais Dk. Magufuli alifariki Machi 17, 2021 na anapumzishwa leo katika makazi ya milele Chato mkoani Geita, huku wananchi wakiwa na huzuni na majonzi makubwa kwa kumpoteza kiongozi huyo aliyedumu madarakani kwa miaka mitano na siku 114.

Licha ya masikitiko yaliyotawala taifa kwa sasa, Rais Dk. Magufuli ameacha zawadi pamoja na ndoto za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ambayo itadumu kwa miaka mingi na kulinufaisha taifa.

Kutamalaki kwa miradi iliyokamilika na inayoendelea kujengwa nchini na maelfu ya wananchi wakijipanga barabarani, kujaa viwanjani huku vilio vikisikika sehemu mbalimbali, kunaleta taswira pana juu ya uongozi wa Rais Magufuli jinsi ulivyowagusa wananchi na vilio vyao ni kulilia tumaini lao.

Rais Dk. Magufuli alipiga vita rushwa na ubadhilifu tangu akiwa waziri hadi alipochukua mamlaka ya kuongoza nchi mwaka 2015, hatua madhubuti alizochukuwa ni pamoja na kuanzisha mahakama maalumu ya kusikiliza kesi za ufisadi unaofanywa na watu mbalimbali nchini

**Rais Dk. Magufuli alipiga vita rushwa na ubadhilifu tangu akiwa waziri hadi alipochukua mamlaka ya kuongoza nchi mwaka 2015, hatua madhubuti alizochukuwa ni pamoja na kuanzisha mahakama maalumu ya kusikiliza kesi za ufisadi unaofanywa na watu mbalimbali nchini**

Aliipa kipaumbele miradi ya maendeleo na kufanikiwa kuitekeleza kwa ufanisi ikiwamo ujenzi wa barabara katika sehemu mbalimbali nchini, uboreshaji viwanda, ukusanyaji mapato, usafiri wa umma ndege.

Pia, kuna kuimarisha sekta mbalimbali, zikiwamo madini, na umeme Bonde la Rufiji, maliasili na italii, elimu, afya, reli ya kisasa ya SGR na utekelezaji wa sera ya viwanda.

Lingine kuna kumaliza tatizo la maji katika baadhi ya miji na vijiji, kutanguliza mbele maslahi ya Watanzania na nchi ambapo hilo lilizaa matunda ya kuinua pato la taifa hadi kufikia uchumi wa kati.

Hadi mwaka 2017, serikali chini ya Hayati Rais Magufuli, ilifanikiwa kuanganisha mamlaka za wilaya takribani 117, vituo vya polisi 129, ufungaji taa za barabarani zinazotumia nguvu za jua, kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 2,571 sambamba na ujenzi wa madaraja.

Alisimamia ilani ya chama chake, CCM iliyosisitiza ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa mbalimbali nchini, pia uongozi ulijikita katika miradi na ikakamilika, na kuanza kutumika, pamoja na kuongeza pato la taifa lakini pia ilisaidia kupunguza tatizo la ajira nchini.

Pia, alifanikiwa kuwaaminisha Watanzania kufanya kazi kwa bidii ndiyo njia pekee ya kumshinda adui njaa pamoja na umasikini sambamba na hilo alimtanguliza sana Mungu, kwa kila jambo alilolifanya katika kutimiza majukumu yake ya kila siku.

Aidha, nchi ilipokumbwa na janga Corona mwaka 2020, alisisitiza umma kuzipa kipaumbele zaidi dawa asilia ili kuweza kujitibu, pamoja na kutumia barakoa za ndani na kuonyesha kutoziamini zilizotoka nje.

Viongozi pamoja na wananchi wana jukumu la kuyaenzi yale mazuri aliyoyafanya kiongozi huyo kwa kuwa wazalendo na kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha maisha ya Watanzania pamoja na kukuza uchumi wa taifa kwa ujumla.

## TANGAZO

**PUMZIKA KWA AMANI**
**Mhe. Dk. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI**

TICTS



Bodi ya Wakurugenzi na Wafanyakazi wa Kitengo cha Makontena Bandarini (TICTS), wanatoa salamu za pole kwa Mh. Rais Mama Samia Suluhu Hassan, Mama Janeth Magufuli, wanafamilia na Watanzania kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa

**Rais wa Tanzania,**
**Mhe. Dk. John Pombe Joseph Magufuli.**

Rais John Pombe Magufuli atakumbukwa kwa maono yake, uzalendo aliouonesha wakati wa utawala wake uliolenga katika kukuza uchumi wa Tanzania na maisha ya watu.

**Raha ya Milele Umpe Ee Bwana na Mwanga wa Milele Umwangazie Apumzike kwa Amani.**

HUTCHISON PORTS
TANZANIA

# Mbaroni tuhuma mauaji bibi kizee

**Na Samson Chacha,** TARIME

JESHI la Polisi katika mkoa wa kipolisi wa Tarime/Rorya, linawashikilia watu wawili wa familia moja kwa tuhuma za mauaji ya bibi kizee, Hulda Magesa.

Wakati watu hao, Mhoni Nyahucho na Chacha Nyahucho wanashikiliwa kwa tuhuma hizo na mahojiano, pia jeshi hilo linawasaka watu wengine wanaotuhumiwa kuhusika na tukio hilo kwa kumteka wakiwa na usafiri usiku na kutoweka naye kisha kumuua na mwili wake kuutelekeza kichakani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tarime/Rorya, Kamishna Msaidizi (ACP) William Mkonda, amethibitisha kumamatwa kwa Nyahucho na kijana wake huku akibainisha kuwa wanaendelea kuwasaka watu wengine huku akiwaomba wananchi kutoa ushirikiano ili wakamatwe.

Alisema Magesa alitekwa Machi 15, mwaka huu, nyumbani kwake mtaa wa Kebikiri na mwili wake kukutwa umetupwa kichakani Machi 22, ukiwa kwenye mfuko wa sandarusi katika Kijiji cha Nyarutu Rozana.

Kamanada Mkona alisema mauaji ya bibi huyo yalitokana na mgogoro wa kugombea uwanja ambao watuhumiwa walijenga wakati Magesa alikuwa mmiliki na baada ya mazishi, wananchi wenye hasira walibomoa nyumba zilizojengwa katika eneo hilo na kuharibu mazao.

Hata hivyo, Kamanda Mkonda amewaonya wananchi kujichukulia sheria mkononi kwa kuwadhuru watu wengine badala ya kufuata sheria za nchi.

"Kama umeshindwa katika kesi kata rufaa (rufani) mahakama ya juu badala ya kujichukulia sheria mikononi. Tunaonya na tutawasaka wote waliohusika katika mauaji hayo ya kikatili," alisema.

Magesa alikuwa na kesi ya kugombea kiwanja na Nyahucho katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Kata na Magesa alishinda na kwamba huenda hicho ni chanzo cha uhasama uliosababisha mauaji hayo.

# Wafugaji kumuenzi JPM kwa kuondoa migogoro

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

KATIBU wa Chama cha wafugaji nchini, Joshua Lugaso, amesema chama hicho kitaendelea kudumisha amani na mshikamano uliopo na wakulima na kuondokana na migogoro ya wafugaji na wakulima ikiwa ni kumuenzi aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Lugaso alisema hayo jana katika kongamano maalumu la kuomboleza kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, lililofanyika katika uwanja wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mvomero.

Alisema katika kipindi cha uongozi wake, Hayati Magufuli alifanikiwa kwa kiasi kikubwa kumaliza mapigano ya wakulima na wafugaji na kurejesha amani kwa jamii hizo mbili na kwamba njia pekee ya kumuenzi ni kuendelea kuyaishi maono yake kwa vitendo."Miaka ya nyuma ilikuwa haipiti siku bila kusikia mahali fulani watu wamekufa kwa sababu ya mapigano ya jamii zetu hizi mbili hasa wialaya hii ya Mvomero na Kilosa, lakini dhamira ya mpendwa wetu Hayati Dk. Magufuli katika kujenga amani ilionekana tangu alipochukua madaraka mwaka 2015, alisema hataki kusikia migogoro ya wakulima na wafugaji na tangu hapo amani ikarejea na kila mmoja akaheshimu shughuli ya mwenzake," alisema Lugaso.

Alisema Hayati Magufuli hakuishia tu kwenye kukemea mapigano ya wakulima na wafugaji bali alitengea wafugaji maeneo ya malisho zaidi ya hekta milioni 2.8 huku ikitarajiwa kuongezeka hadi kufukia hekta milioni sita katika kipindi cha mwaka 2020/2025.

Loata Ole Sanare, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro alisisitizia umuhimu wa kuendeleza ushirikiano hasa katika kipindi hiki taifa linapogubikwa na simanzi na kumtanguliza Mungu kulinda amani.

Alisema katika ziara ya mwisho aliyoifanya Hayati Magufuli mkoani Morogoro Februari 12, mwaka huu alitoa pongezi nyingi baada ya kushuhudia hali ya utulivu katika wilaya za Mvomero na Kilosa tofauti na ilivyokua awali wakati migogoro imeshamiri.

"Alitupongeza sana viongozi na wananchi wa Morogoro kwa kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji kwa sababu aliponiteua kuwa mkuu wa mkoa jambo alilosisitiza ni kumaliza hali ile ambayo alisema inamsumbua sana akili yake, kwa hiyo tuendelee kushirikiana kutunza amani hii ila hata huko alipo apumzike kwa amani akiamini Morogoro ipo salama," alisema Sanare.

Mkuu wa Wilaya, Albinus Mgonya, alisema madhumuni ya kongamano hilo ni kuwapa fursa watu ambao hawakupata nafasi ya kuaga mwili wa mpendwa wao katika maeneo yaliyoelekezwa na kutoa wito kuendeleza aliyoyasimamia katika uongozi wake.



Mwendesha pikipiki, akiwa ameisheheni mzigo wa mkaa katika Kijiji cha Msanga, Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani hivi karibuni, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hosea aeleza kwanini anatosha TLS

**Na Elizabeth Zaya**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Dk. Edward Hoseah, ametaja sababu tatu zinazomsukuma kugombea urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).

Katika taarifa ya maandishi na video aliyorushwa kwenye ukurasa wake wa Twitter, alitaja sababu ya kwanza ni kuhakikisha analeta chachu ya mabadiliko ndani ya chama hicho.

Dk. Hoseah ambaye aliongoza TAKUKURU kuanzia mwaka 2006 hadi 2016, alisema atahakikisha anasaidia wanasheria wengi, hususani vijana, ambao wanatumia gharama kubwa kuhuisha vyeti vyao, kumaliza shida hiyo.

Aidha, alisema sababu ya tatu ni kutumia uzoefu wake kuhakikisha TLS inapiga hatua nzuri zaidi na kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

"Nina sababu kuu tatu za mimi kugombea nafasi hii, kwanza ni haki yangu kidemokrasia. Lakini kubwa nataka kuleta uzoefu wangu katika maisha ambayo nimepitia na la msingi ni kwamba chama hiki kwa sasa kinahitaji kuwa na mtu mwenye uzoefu," alisema Dk. Hoseah.

Kwa mujibu wa Dk. Hosea, kugombea nafasi hiyo ni haki yake kidemokrasia na ameitumia vyema.

"Nimefanya kazi serikalini zaidi ya miaka 36, kwa hiyo naamini uzoefu huu utakuwa ni mchango wangu kwa TLS ili kuongeza chachu ya kuyafikia malengo yake yaliyowekwa kisheria.

"Kwa sasa chama hiki kinahitaji kuwekeza, ni muda sasa tuanze kuwekeza, wanachama wengi ambao ni vijana wanalipa hela nyingi ku'renew' (kuhuisha) vyeti vyao katika ku-'practice' (kufanya kwa vitendo). Uongozi ni wito, muda umefika sasa ninawiwa mwaka huu 2021,nitakifanya kipige hatua zaidi kwa kuongeza value (thamani)," alisema.

Duru mbalimbali zinaeleza kuwa huenda uchaguzi wa TLS mwaka huu, ukawa mgumu zaidi kwa nafasi ya urais kwa sababu wagombea katika kinyang`anyiro hicho wengi ni wazoefu.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Uchaguzi huo, Mariam Othman, alisema wagombea watano wamepitishwa kugombea katika nafasi hiyo. Mbali na Dk. Hoseah, wengine wanaopambana kupokea kijiti cha Dk. Rugemeleza Nshala ni Flaviana Charles, Shehzada Walli, Albert Msando na Francis Stolla.

Kwa mujibu Mariam, wagombea hao watapigiwa kura April 16, mwaka huu, na matokeo kutangazwa siku hiyo hiyo, katika uchaguzi utakaofanyika jijini Arusha.

# TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**WAKALA YA BARABARA TANZANIA**

# LALA SALAMA MWANAMAGEUZI MAHIRI



**HAYATI DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI 1959-2021**

**Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, Mtendaji Mkuu, Menejimenti na Wafanyakazi wa TANROADS, kwa masikitiko makubwa tunaungana na Watanzania wote katika mazishi ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo siku ya Ijumaa tarehe 26 Machi, 2021.**

**TANROADS tutaendelea kukuenzi daima, kwa kuifuata falsafa yako ya 'Hapa Kazi Tu' na kufanya kazi kwa bidii, Juhudi, Maarifa, Kasi na Weledi Hususan katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara, Madaraja na Viwanja vya Ndege kwa Maendeleo ya Taifa Letu.**

**Aidha, tunatoa pole nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, Mama Janeth Magufuli na Familia, na Watanzania wote kwa msiba huu mkubwa wa Taifa.**

**Pumzika kwa Amani Shujaa wetu, Kiongozi Jasiri na Shupavu, Mwanamageuzi Mahiri, Mzalendo na Mwanamwema wa Afrika. Tutakukumbuka na Kukuenzi Daima.**

**BWANA AMETOA, BWANA AMETWAA, JINA LA BWANA LIHIMIDIWE. AMINA.**

**TANROADS Makao Makuu:** Ghorofa ya1-3, 10 Barabara ya Shaaban Robert / Garden Avenue S.L.P 11364 Dar es Salaam
BaruaPepe: Tanroadshq@tanrods.go.tz. www.tanroads.go.tz

***MIUNDOMBINU BORA YA BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE KWA MAENDELEO YA TAIFA***

# Club yapunguza mimba za wanafunzi

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

CLUB ya wanafunzi katika Shule ya Sekondari Salawe Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, ambayo inajihusisha na utoaji wa elimu ya makuzi na afya ya uzazi, imesaidia kupunguza tatizo la mimba za wanafunzi shuleni hapo.

Mkuu wa shule hiyo, Faraja Mbilinyi, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari ambao wanatekeleza mradi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Mbilinyi alisema mwaka 2019 alipohamishiwa shuleni hapo kikazi, alikumbana na tatizo la wanafunzi 19 kupewa ujauzito na kuacha masomo, lakini baada ya kuanzishwa club ya wanafunzi, mimba za wanafunzi zimepungua na kutokea tatu kwa mwaka tofauti na zamani.

"Hatua ambayo tuliichukua kama shule kukabiliana na tatizo hili la mimba za wanafunzi ni kuanzisha club kwa ajili ya kutoa elimu ya makuzi, afya ya uzazi na madhara ya kujamiiana katika umri mdogo, hali ambayo imesaidia kupunguza kasi ya mimba shuleni hapo," alisema Mbilinyi.

Mmoja wa wanafunzi, Paulina Fabian, anayesoma kidato cha nne, alisema club hiyo imesaidia wanafunzi wengi kujitambua pamoja na kutoa taarifa pale wanapokuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili, na hatimaye wahusika kuchukuliwa hatua mapema kabla ya kuleta madhara.

Diwani wa Kata ya Salawe, Joseph Buyugu, alisema katika kutatua tatizo hilo la mimba za wanafunzi, walikaa na viongozi wa serikali na kupitisha mikakati ikiwamo kuwakamata wahusika na kuwawajibisha kupitia jeshi la jadi Sungusungu pamoja na kuwatenga kwenye kijiji, hali ambayo imesaidia kupunguza mimba za wanafunzi.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwataka wanaume kuacha tabia ya kurubuni wanafunzi na kujamiiana nao, bali watafute wanawake wenye rika lao ndio washiriki nao tendo hilo na siyo watoto wa shule, huku akionya serikali itaendelea kuwashughulikia ambao watawapa ujauzito wanafunzi.



Wanawake wakichimba msingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Shule ya Msingi Karubugu, Kata ya Mugango, wilayani Musoma, mkoani Mara juzi, ikiwa ni kuchangia nguvu kazi yao katika kazi hiyo. PICHA: MPIGAPICHA WETU

## Vipodozi, vyakula visivyofaa vyaondolewa sokoni

**Na Felix Andrew**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Kusini limeondoa vipodozi vyenye viambatasumu (Hydroquinon, madinitembo na zebaki) pamoja na vyakula vilivyokwisha muda wa matumizi vyenye thamani ya Sh. 1,350,000.

Hayo yalibainishwa na Mkaguzi wa TBS Kanda ya Kusini, Buliro Magesa, alipokuwa alizungumzia usajili wa shirika wa maduka ya dawa na vipodozi katika kanda hiyo.

"TBS tunaendelea na usajili wa maeneo ya kuuzia vyakula, vipodozi, migahawa pamoja na maghala ya kuhifadhia bidhaa hizo lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa mwananchi wa kawaida anapata bidhaa bora na salama wakati wote," alifafanua.

Alisema shirika limekwisha sajili maduka ya vipodozi, vyakula na migahawa 601 katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma tangu lilipoanza kutekeleza jukumu hilo Julai 2019.

Magesa, alisema juzi kuwa katika ukaguzi uliofanyika kati ya Machi 03 na Machi 17, mwaka huu, Manispaa ya Lindi, Kilwa na Mtama mkoani Lindi, shirika limesajili maduka ya vipodozi, chakula na migahawa 41 hivyo kufanya idadi kufikia 601 kutoka 560.

Alisema Kanda ya Kusini imekwishapokea maombi 1,089 na kati ya hao wenye vibali vya usajili ni 601 na wasio na vibali ni 488.

Wakati huo huo, Ofisa Uhusiano Mkuu wa TBS, Roida Andusamile, alisema shirika litaendelea kusajili na kuthibitisha ubora wa bidhaa mbalimbali ikiwamo utekelezaji wa jukumu mojawapo la msingi la shirika kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Viwango Namba 2 ya mwaka 2009.

Alisema shirika litaendelea kuwahimiza wenye maduka ya vipodozi vyakula na migahawa kuhakikisha kuwa wanapata usajili na kuuhisha mara moja muda wa usajili unapokwisha.

Aliongeza kuwa wananchi wanapaswa kuelewa kuwa shirika limejikita katika kuwezesha biashara sambamba na kumlinda mlaji hivyo katika kutekeleza jukumu hilo bidhaa zinazouzwa sokoni ni lazima zikidhi matakwa ya kiwango na kutoleta madhara kwa mtumiaji.

"Tunawasihi wafanyabiashara kulitumia shirika ipasavyo kwani limejikita katika kutoa huduma na kuwasaidia kuondoa vikwazo vya kibiashara vinavyotokana na kutozingatia viwango," alisisitiza Andusamile.

## Waziri Mkenda ataka ubunifu kuleta mageuzi kwenye kilimo

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, juzi alizitaka taasisi chini ya Wizara ya Kilimo kuongeza ubunifu ili kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo na pia kuchochea ukuaji wa sekta ya viwanda kilimo hapa nchini.

"Ubunifu huu wa kuanzisha mradi huu wa Kizimba 'Business Model' ni kitu cha kuigwa na taasisi nyingine katika jitihada ya kuleta mageuzi ya kweli katika sekta ya kilimo. Kilimo kinachangia asilimia 28 ya pato la taifa," Prof. Mkenda alisema mjini hapa.

Akizungumza muda mfupi baada ya kuzindua mradi huo unaolenga kuvutia na kuwahamasisha wanaohitimu vyuo kujikita katika kilimo biashara, Prof. Mkenda, alisema mageuzi katika sekta ya kilimo yatasaidia, pamoja na mambo mengine, kupunguza umaskini miongoni mwa Watanzania.

"Sambamba na kuzinduliwa kwa mradi huu, napenda kutoa wito kwa benki za biashara na taasisi zingine za kifedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana wanaojishughulisha na kilimo biashara ili kuharakisha mageuzi katika sekta ya kilimo," alisisitiza.

Mbali ya kukipongeza Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Ushirika wa Wajasiriamali Wahitimu wa SUA (SUGECO) kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika sekta ya kilimo, Waziri Mkenda aliwataka Watanzania kuenzi na kuchangamkia fursa za mafunzo zinazotolewa na taasisi hizo ili waweze kushiriki vizuri na kuleta mageuzi katika kilimo.

Katibu Mkuu mstaafu wa Wizara ya Kilimo, Peniel Lyimo, mbali ya kuupongeza mfumo wa kilimo unaoratibiwa na SUGECO, alilitaka taifa likiangalie kilimo kwa jicho la pekee. Lyimo ni muhitimu wa fani ya kilimo kabla ya SUA. Ni muhitimu wa Kitivo cha Kilimo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Kilimo kinahitaji pesa kama sekta ya kiuchumi. Lakini kikilinganishwa na sekta nyingine, kilimo kinabeba tishio sana za hasara (risks) kuliko sekta nyingine za kiuchumi. Kilimo kinahitaji mtaji mkubwa kufanikiwa, ndiyo maana serikali imeanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo," alisema Mzee Lyimo.

Alisema mradi wa Kizimba utachochea ukuaji wa viwanda vya kilimo na kushauri uwafikie wakulima wengi nchini kwani unalenga kuongeza uzalishaji na kupanua wigo wa masoko.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Prof. Raphael Chibunda, alisema chuo kitaendelea kushirikiana na wizara ya kilimo kusukuma na kuubadilisha mfumo wa kilimo ili wakulima wajikite katika kilimo biashara. Chuo, alieleza, kimeanzisha mashamba ya kilimo biashara kwenye maeneo yote ya chuo.

Alisema SUGECO imefundisha kwa vitendo zaidi ya vijana 100 stadi za kilimo biashara kwa kutumia vitalu nyumba. Hatua hiyo, alieleza, imechangia kukuza ajira na kipato kwa vijana.




UCHUMI

# Hizi hapa hatua zilizomvusha kufikia Uchumi wa Kati, Tanzania ya Viwanda

**Na Peter Orwa**

NI miaka sita ilipita, Tanzania ikitekeleza sera na mikakati ya kiuchumi, chini ya Rais Dk. John Magufuli, ambaye sasa hayuko tena duniani, nafasi yake ameshakabidhiwa aliyekuwa Makamu wake, Samia Suluhu Hassan.

Wote hao wanatoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), hivyo kuna hoja kwamba wanatekeleza mtazamo na mkakati wa pamoja unaoanzia katika ilani yao ya uchaguzi, sera na itikadi ya pamoja, ndio mwongozo rasmi wa kisiasa ulivyo, mgombea anayeshinda anawajibika na ilani hiyo.

Juzi katika mwendelezo wa makala hizi ilikuwa na ufafanuzi wa siasa ya uchumi anayotumia Rais Dk. John Magufuli, kwamba inaangalia mlengo wa kushoto kiuchumi au siasa za kijamaa, akishikilia wiko wa mzizi wa itikadi za mwasisi wa taifa, Mwalimu Nyerere.

Katika mtazamo huo wa kiuchumi, ilibebeshwa tafsiri ambayo mmoja wa wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Alfred Lokuji, anayefafanua: "Serikali inakuwa sehemu ya umma, kamwe haiwezi kubaki kando watu wake inaingilia kati kuwanusuru kutoka kuelemewa na gharama za nguvu ya soko."

Vivyo hivyo, katika dhana hiyo ya uchumi ambayo Rais Dk. Magufuli alisifiwa nayo sana, wasomi wataaluma wake wanautafsiri katika dhana kuwa "namna mtu, taasisi, mamlaka, au kikundi cha watu kinajipanga kufaidika kwa kiwango kikubwa, rasilimali kidogo ili kujinufaisha kwa mahitaji yake yenye kipaumbele."

Mathalan, namna mtu anavyojipanga kutimiza mahitaji yake muhimu kama chakula, malazi na ada ya shule kwa watoto kupitia mshahara kidogo anaoupata.

Ndani ya mtazamo huo, ndio Rais Dk. John Magufuli, alishuhudiwa kufanya mengi mazito katika uongozi wake, jambo linalombebea heshima kubwa leo anapopumzishwa katika nyumba yake ya milele, baada ya kuacha kishindo cha miaka mitano na miezi kadhaa kuitumikia taifa ngazi ya juu kabisa ya serikalini, akiwa na miaka zaidi ya 20.

**ALIENDAJE KIUCHUMI?**

Katika utekelezaji huo, Rais Dk. Magufuli, muda wote alibeba tafsiri kuu tatu katika nyendo zake kiuchumi, kwamba: Nchi kiujumla inazalisha zaidi; inapunguza gharama zisizo na msingi kwa umma; na kusonga kufikia hatua yenye mafanikio kuzalishaji, ambayo nyayo za taifa sasa zimegusa 'Uchumi wa Kati.'

Mtazamo mkuu katika yote, tangu aanze nayo kiuchumi ni kuiona Tanzania inafikia Uchumi wa Viwanda, huku ikiufuta umaskini wa mtu mmoja mmoja. Hapo ndio kunakozaa msamiati wake katika hotuba "Nimeamua 'ku-sacrifice' (kujitolea) maisha yangu kwa ajili ya Watanzania."

Mara tu baada ya kuapishwa kwa mara ya kwanza, wakiwa wawili na Makamu wakati huo, Samia Suluhu Hassan, Dk. Magufuli aliongoza timu yake kiserikali akiwa na namna nyingi ya kufanikisha mustakabali wa uchumi nchini.

Eneo mojawapo ni katika watumishi wa serikali, akiwataka kuwajibika kwa kadri ya thamani ya uwezo wao katika ujuzi, taaluma na kutumia muda wa kuwapo kazini kwa kadri inavyowezekana.

Hilo lililenga katika kuhamisha na baadhi ya maeneo kuwa ya kisheria, ikiwamo marufuku ya maeno ya ulevi kufunguliwa mapema na uchezaji wa 'pool; muda wa kazi.

Dhana kuu hapo iliyojengwa hapo ni nidhamu ya kazi na kwa mfanyakazi mmoja mmoja, hata hivi sasa imebadilisha hulka katika nafasi ya utumishi wa umma katika ufanisi mkuu; nidhamu na kuzingatia muda, aliupa umuhimu wa kipekee wakati wote katika utendaji wake.

Hapo kuna ushuhuda, pale mfanyabiashara alipotoa maoni redioni kwamba zamani alitumia zaidi ya wiki kupata leseni, sasa ni ndani ya siku mbili.

Hadi anafariki alikuwa na misisitizo wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), kufanya mageuzi makubwa ya tija, ikiwamo kuhakikisha taratibu za muda zinachukua muda mfupi, ili kuvutia wawekezaji wengi.

Ni mara nyingi alipigana binafsi katika mikakati na mbinu mbalimbali za kufugua milango na hata wawekezaji wengi wamejitokeza katika sekta ya viwanda na kumekuwa na ujio mkubwa, miji midogo kama Mkuranga, sasa mapori yake ni maarufu kwa viwanda Katika madini, aliweza kuhamasisha na wakati huohuo, aliweka udhibiti wenye manufaa kwa Watanzania, mifano ya kihistoria ikibaki katika udhibiti wa makinikia na ujenzi wa ukuta machimbo ya madini Tanzanite, huko Mirerani, ikiingizia taifa kipato kikubwa na mamilionea, akiwapo wa mfano Laizer.

Sambamba na hayo, mikakati iliyopo ni kujengwa kiwanda cha kuchakata madini, ili sehemu kubwa ya thamani ya madini ibaki nchini na kifuta hadithi ya makinikia.

**ALIVYOFUATILIA**

Dk. Magufuli alilitimza agizo lake kwa ziara za ghafla alipotinga katika wizara kadha nchini, kukagua mwenendo wa watumishi wanavyowajibika.

Ni namna ambayo, pia kiongozi huyo alichukua muda mrefu akisaidiana na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, katika kusaka na kuchuja majina kwa wale waliomfaa kuunda Baraza la Mawaziri, kufanikisha majukumu yake.

Baada ya kukamilisha hilo, aliweka wazi namna angetimiza falsafa ya 'kutumbua' kwa mtumishi aliye kinyume na mwenendo unaodhamiriwa na ilifanyika kwa mawaziri na maofisa waandamizi kama vile wakurugenzi katika halmashauri mbalimbali za nchi.

Huku nadharia ya kuwajibika ikiwa imepamba moto, katika serikali yake alibeba nadharia iliyoko rasmi katika uchumi kwamba 'thamani ya fedha inayotumika' ifanane na gharama halisi.

Vivyo hivyo, kukasimamiwa pale kinachonunuliwa kinapaswa kubeba sifa zake tano za usahihi kitaaluma; katika idadi ya vitu au kiasi cha huduma iliyolipiwa, bei sahihi, ubora, muda unaonuliwa na chanzo sahihi.

Katika hilo alikuwa mkali sana na hata mbaya, kwa wahusika katika fani kama za ununuzi, mauzo, fedha, mipango na wasimamizi wa miradi.

Ili kuendana na uhalisia sahihi, Dk. Magufuli alibadili mfumo wote wa malipo, akitaka kupitia benki, vivyo hivyo kukaanzishwa Mfumo Malipo ya Kielektroniki Serikalini maarufu (Gepg), huku Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ikiwa na mfumo wake wa kieletkroniki, maarufu EFD.

Alikuwa na mfumo upi? Ndio katika namna ya simulizi ya Mwalimu Julius Nyerere, kati ya mwaka 1964 hadi anaondoka, aliamini kwa kuwa na Tanzania ya Viwanda na hasa kuanzia na viwanda vya kutengeneza mahitaji ya msingi, baadaye viwanda vikubwa vidogo vya mwaka 1973 , kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) na badaa ya mwaka 1975, mkakati wa miaka 20 kuwa na viwanda mama ulioishia njiani.

Kwa watumishi wa umma walioshikwa kupitia Sheria ya SCOPO, mwaka 1969, ikaendana na kuundwa Tume ya Rais ya Kusimamia Mashirika ya Umma, haikuwa tofauti sana na kinachofanywa na kitengo cha Utumishi, kilichopo chini ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma



Wajumbe wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), walipokuwa nchini kwenye mkutano wa mwaka walipotembelea kiwanda kipya kilichoko, Mkuranga. Ni matunda ya juhudi zake Dk. John Magufuli, ambaye alikuwa mwenyekiti wa jumuiya hiyo wakati huo. **PICHA: MTANDAO**

# MJI CHATO ILIVYOSHIKWA NA BUTWAA 'TUMEPOTEZA'

- Bodaboda ukutani mwake wabaki hawaamini
- Aliyekuwa anamkopesha 'azimia' uaminifu ule
- Kuingia siasa tu, ghafla Chato ikafurika wakazi
- Lami na taa kibao; wiki nzima Geita ni simanzi

**Na Richard Makore, CHATO**

WENGINE wanamwita shujaa wao na wapo wanaotamka neno moja tu, 'Tumepoteza', huku kundi la lingine la wana Chato linasema "bila Hayati John Magufuli, Wilaya ya Chato iliyopo mkoani Geita itarudi nyuma miaka 20."

Ni maneno ya wana Chato ambao baadhi wamezaliwa hapo, lakini wengine walifika hapo kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za kimaisha.

Wakazi wa Chato ukizungumza nao hawaachi kutamka bayana kwamba, hayati Dk. Magufuli alikuwa msaada mkubwa kwao.

Hakuna anayesema kwamba Hayati Dk. Magufuli alikuwa akiwapa fedha moja kwa moja, kuwalisha au kulisha familia zao.

Wengi wao wanachotamka, ambacho hawawezi kukisahau kwake ni kuwapo maendeleo ya vitu, ikiwamo barabara za lami zenye taa mpaka uchochoroni, lakini pia utulivu na mazingira mazuri ya kufanyia biashara.

James Andrew ni Mwenyekiti wa Umoja wa Waendesha Bodaboda katika wilaya ya Chato, anasema, Hayati Magufuli aliwajali kwa kuwatembelea kila alipofika nyumbani kwao kwa mapumziko.

Andrew anasema kituo chao cha Bodaboda kipo jirani na ukuta wa nyumba ya Hayati Dk. Magufuli, lakini hawajawahi kusumbuliwa na mtu ili waondoke hapo.

Pia, kingine anachokitaja ni kabla Magufuli kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mji wa Chato haukuwa na wakazi wengi kama ilivyo sasa.

Andrew anasema kiongozi huyo alijitahidi kupigania upatikanaji wa huduma muhimu kwao, zikiwamo maji, umeme, hospitali, uwanja wa ndege pamoja kuboresha miundombinu ya barabara za lami kila mtaa.

> **"Hayati Dk. Magufuli, ambaye anawekwa katika nyumba yake ya milele leo hii, ana tafsiri kama ilivyo ya wenzake wa kimataifa, anabaki katika alama kuwa ni mtu shujaa, mkombozi, baba, ndugu na mtu aliyewapenda na kuwajali katika maisha yao.**



Rais John Magufuli, namna alivyoishi na wakazi wa Chato, pindi awapo likizo. Hapo akijiunga katika kijiwe cha Kahawa.. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### MFANYABIASHARA ALIYEMKOPESHA

Kwa upande wake, mfanyabiashara wa nyumba za kulala wageni, Mwita Chacha, anasema walifahamiana na Hayati Dk. Magufuli wakati huo akiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na baadaye Waziri kamili enzi wa utawala wa hayati Benjamin Mkapa

Anasema, Dk. Magufuli hakupenda dhuluma na kwamba enzi hizo alikuwa akimuuzia vifaa vya ujenzi kwa mkopo mpaka vya thamani ya Sh. milioni 15.

Chacha anasema, Dk. Magufuli alipotoka Dar es Salaam, alikuwa anamwita na kumpa fedha zake, huku akimtaka asaini kwenye daftari maalum kuwa amepokea kiasi hicho.

Anasema, wakati huo ndiyo mji wa Chato ulipoanza kupata mabadiliko makubwa ya kiuchumi na watu wakaanza kuongezeka, huku biashara zikianza kuboreka.

### HUZUNI YAO

Wananchi wengi wa Chato, wanahuzunika na mara kadhaa utawakuta katika vikundi vikundi na ukiwasalimia na kuwapa pole, wanakwambia tumempoteza Baba na mtetezi wetu.

Ujumbe wao ni kwamba, walimuona katika tafsiri ya Baba wa Chato na mtu ambaye aliyekuwa amebeba watu wengi mgongoni mwake katika uhai wake.

Swali wanalojiuliza sasa wana Chato ni moja tu, je Chato itapata mbadala wa kuenea kiatu chake? Na je, baadhi ya vitu alivyovianzisha Hayati Dk. Magufuli na kuvisimamia, vitaendelezwa?

Ni aina ya maswali ambayo Nipashe ilibaini yametawala mijadala ya vikundi na minong'ono ambayo kwa baadhi wanaishia kulia, wakishindwa kuzungumza tena, hata kufikia kutopenda kusikia mjadala wa kisiasa hivi sasa.

Hayati Dk. Magufuli, ambaye anawekwa katika nyumba yake ya milele leo hii, ana tafsiri kama ilivyo ya wenzake wa kimataifa, anabaki katika alama kuwa ni mtu shujaa, mkombozi, baba, ndugu na mtu aliyewapenda na kuwajali katika maisha yao.

### KALEMANI AJITWIKA JUKUMU

Mbunge wa jimbo la Chato, Medard Kalemani, akizungumza na wazee wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Geita, anaahidi kwa kujibebesha jukumu kwamba, vitu vyote vilivyoanzishwa na Hayati Dk. Magufuli atavisimamia.

Anawatoa hofu wanaCCM wenzake kwamba, analifahamu vyema jimbo la Chato, hivyo yuko katika rai kwamba atahakikisha anafuata nyayo za hayati Dk.Magufuli kama zilivyo.

Katika hilo, anasema njia pekee ya kumuenzi Hayati Dk. Magufuli ni kuendeleza upendo,mshikamano na ushirikiano kwa wana Chato kwa ujumla

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge Ngara, Severine Niwemugizi, anamtwisha heshima ya kuwa muumini wa kweli katika kanisa hilo, akidodosa historia yake.

Kiongozi huyo wa dini, anaeleza kwamba, Dk. Magufuli alibatizwa katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Jimbo la Rulenge na kwamba safari yake ya kiimani inaishia kanisani hapo, kwa maombi maalum, kisha taratibu zingine za kiitifaki, zikiwako za kumuaga

### ALIKOTEKA NYOYO ZAO

Hayati Dk. Magufuli anaonekana kuteka nyoyo za wananchi wa Kanda ya Ziwa, ambako ana historoa nao mbali na urafiki, asilia ya kimafilia kwake na mkewe, alikozaliwa, kusoma, kuanzia kazi yenye mafanikio katika Sekondari Sengerema na Ushirika Nyanza, undugu wa karibu kabla na bada ya urais.

Ni katika namna ambao sura ya undugu huo ulikuwa bayana, waratibu wa safari ya kumuaga waliwapa nafasi Kanda ya Ziwa na wananchi wake, waliuaga mwili wake katika mikoa ya Mwanza na Geita.

Uchunguzi wa Nipashe ndani ya mitaa ya mji wa Geita, ulishuhudia mwendelezo wa nyimbo za kabila la kisukuma ambao ndio wenyeji wakuu, zilizokuwa zinapigwa kwenye kampeni za uchaguzi mkuu mwaka jana.

### MJI WA GEITA

Ni aina ya nyimbo zenye utashi wa kuvuta hisia na baadhi ya watu huanza kutokwa machozi wakimkumbuka mkombozi wao, aliyeaga dunia.

Pale, mara baada ya aliyekuwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alipotangaza kifo hicho, mji wa Chato umekuwa kimya na wakazi wakijiuliza maswali ambayo mara moja walijuliza "Itakuwaje siku ya Ahamisi (jana) ya kumuaga mpendwa wao mjini Chato?"

Hata hivyo, Nipashe ambayo imepiga kambi mjini Chato, ilishuhudia jana namna jambo hilo lililendeshwa kwa amani na utulivu, katika mpangilio maalum kwenye uwanja uliopewa jina lake mjini Chato.

Leo hii ndio siku ya mwisho ambayo Hayati Dk. John Magufuli, anawekwa katika nyumba yake ya milele tangu kifo chake siku tisa zilizopita, jijini Dar es Salaam, na kuagwa katika jiji hilo, Dodoma alikoishi, Unguja, Mwanza, Geita na nyumbani kwao Chato, jana. AMINA

## SHAIRI KUMUENZI JPM

### RAIS ULALE PEMA

1 Woi, kiza kimetanda,mwenzenu nashika tama,
Moyoni sina amani,akili imenikwama,
Ametuacha kwa nini, kiongozi wa heshima?
Rais ulale pema, John Pombe Magufuli.

2 Nilipopata habari,amepoteza uzima,
Nilizimia Johari,simanzi ilinizima,
Katuacha jemadari,hakika huko kwauma,
Rais ulale pema, John Pombe Magufuli.

3 Taifa la Tanzania,tunalia nchi nzima,
Ni vigumu kutulia, ni kubwa hii simanzi,
Muhali kuvumilia, hatuna moyo wa chuma,
Rais ulale pema, John Pombe Magufuli.

4 Uli mchapakazi, mwadilifu kwa huduma,
Uliwakomoa wezi, mafisadi wenye wenye njama,
Kusisitiza uwazi, na kufanya kazi njema
Rais ulale pema,John Pombe Magufuli
.
5. Bara letu Afrika, na watuwe bara zima.
Popote ulitambulika, uongozi wako mwema,
Marais wamefika, kudhihirisha heshima,
Rais ulale pema, John Pombe Magufuli
.
6. Ingawa umeondoka, amekutwaa Rahima.
Daima tutakukumbuka,ulotenda na kunena
Kwa dhati tulizishika, ulohimiza umma,
Rais ulale pema, John Pombe Magufuli.

7. Twasifu mola mpaji,tulizani tumezama,
Kumwinua mfariji, Samia Suluhu mama,
Atakidhi mahitaji, yetu tulinayo umma,
Rais ulale pema, John Pombe Magufuli.

8. Bi Janeth Magufuli, na wana pole mama,
Hakika kifo ni nduli, twajua kimewachoma,
Mungu awatunze kweli, awapozeni mitima,
Rais ulale pema, John Pombe Magufuli.

9. Wenzetu mlo Geita, mkoa huo mzima,
Hasa Chato hadi kata, majonzi yanawauma,
Pole zangu mkipata, ni furaha yangu jama,
Rais ulale pema, John Pombe Magufuli.

10. Kaditama nimefika,ni mwisho hapa nime-koma,
Kazi kwako Mhariri, kuchapisha fanya hima,
Hebu fanya kwa hiari, nakuomba kwa heshima,
Nimwambie lala pema, John Pombe magufuli.

**MTUNZI: Johari Mutani**
**Simu: +255 653058666**
**DODOMA**

### WAKENYA TWAOMBOLEZA

1 Rais Mama Samia, ya mgambo ululiza
Jirani tumesikia, na Kenya twaomboleza,
Kwa uchungu tunalia, sisi tumeona giza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli

2 Poleni Watanzania, Magufuli ku'poteza,
Hakika hiyo tanzia, sote imetuumiza,
Kifo kilimvamia, mletaji wa mwangaza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

3 John Pombe Magufuli, alikua na ruwaza
Ruwaza yenye adili, tena kuitekeleza,
Aliifata kamili, na katu hakuteleza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

4 Ukatokea mkosi, kipindi hakumaliza,
Mkondo ukawa basi, na hilo linatuliza,
Alipokonywa nafasi, karudi kwa Muweza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

5 John mwanalugha nguli, alichapa kiingereza,
Na lugha ya Kiswahili, ndo hasa alihimiza,
Alilinda kamili, kaitunza na kukuza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

6 Na sisi wakereketwa, wa lugha aloikweza,
Nyuma hatwezi kuachwa, katika kuomboleza,
Wajibu hutekelezwa, kuhepa hatutaweza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

7 Sote tu wapita njia, na hatuna miujiza,
Dunia kukwamilia, hatuna huo uweza,
Mwisho twe'nda kwa Jalia, atatuita Muweza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

8 Twamshukuru Maanani, tayari amemwingiza,
Kiongozi wa thamani, huyu atawaliwaza,
Ndiye Samia Hassan, vyema atawaongoza
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

9 Huyu Samia Suluhu, urais anaweza,
Yeye atakua Nuhu, meli atawaingiza,
Atailetа suluhu, mambo yakiwatatiza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

10 Ibariki Tanzania, uibariki Muweza,
Nchi ilo na raia, ambao wanapendeza,
Wakati wanapolia, upate kuwatuliza,
Kifo tunaomboleza, cha Rais Magufuli.

**MTUNZI: THOMAS K.S KOSGEI**
**Simu: +254 720001820**
**Kijijini Koisagat,**
**Fort Ternan,**
**KERICHO, KENYA.**



Mitaa ya mji wa Chato, ikiwa na taa za kuongoza magari zilizowekwa tangu Dk. John Magufuli, alipokuwa mbunge wao.

# Miradi; Hifadhi, Bwawa la Nyerere, zawadi alizowaachia Watanzania

**Na Moshi Lusonzo**

PORI tengefu la Selous ni maarufu Duniani kutokana kuwa na utajiri mkubwa wa maliasili wakiwamo wanyama pori, madini na mito inayotiririsha maji mwaka mzima.

Ni wazi Selous yenye ukubwa wa kilomita mraba 54,600 ina utajiri wa kipekee, lakini kwa miaka mingi haukuwa ukifahamika kutokana na kukosa mikakati madhubuti ya kuilinda, badala yake wageni walingia na kutoka katika pori hilo wakibeba rasilimali muhimu bila kikwazo.

Inaaminika Selous ndio ilikuwa pori la akiba kubwa zaidi Duniani, ambalo lilijumuisha mikoa ya Pwani, Morogoro, Ruvuma na Lindi.

Hata hivyo, Rais hayati Dk. John Pombe Magufuli, amelipa thamani pori hilo kwa kuamua kuligawa upya ili kuwanufaisha Watanzania wengi.

Katika mgawanyo huo sehemu ya eneo Kilomita mraba, 30,893 imeanzishwa hifadhi kubwa ya Taifa inayoitwa Julius Nyerere.

Sehemu ya pori hilo, kunajengwa bwawa kubwa la maji ambalo litakapokamilika ujenzi wake litaweza kuzalisha umeme zaidi ya megawati 2000.

Tamko la kuanzisha mbuga hiyo lilitolewa na Hayati Dk. Magufuli, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa mto Rufiji mkoani Pwani, mwezi Juni mwaka 2019.

"Eneo la Selou ni eneo kubwa ambalo linachukua takribani kilomita 50, hivyo ni lazima Wizara igawanye eneo na kuanzisha hifadhi ya Taifa ili kukidhi mahitaji ya utalii na kukisaidia kizazi kijacho kuendelea kuenzi mambo ambayo ameyafanya baba wa Taifa," alisema Hayati Magufuli.

Alitaka eneo hilo ambalo lilihodhiwa na kampuni 47 za uwindaji litengwe na kuwa hifadhi ili kuimarisha utalii na kuvutia watalii wengi katika mbuga hiyo

Aliikumbusha Wizara ya Maliasili na Utalii, kuangalia maeneo kama hayo ya vitalu vya uwindaji kuhakikisha serikali inafaidika na katika kuhakikisha hifadhi hiyo inafikika kwa urahisi, akaagiza barabara ya kutoka Fuga yenye kilomita 60 kujengwa kwa kiwango cha lami.

Licha ya eneo hilo kuwa kituo muhimu cha utalii pamoja na uzalishaji umeme, alitaka kuwa kitovu cha ajira kwa wananchi wanaoishi mikoa ya Kusini.

Katika mradi wa uzalishaji umeme pekee utakapochochea maendeleo katika sekta ya viwanda, ambayo wewekezaji wataweza kupata umeme wa uhakika. wenye kuaminika na kwa bei nafuu, ili kuzalisha bidhaa bora na za bei rahisi.

Kabla ya kifo chake Rais Dk. Magufuli, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alikiri ndoto ya kuenzi mambo makubwa ya Baba wa Taifa, Mwalimu .Julius Nyerere ikiwamo utekelezaji wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme katika maporomoko ya maji ya Mto Rufiji ni jambo la kujivunia.

Waziri Mkuu, anasema kampuni zinazojenga mradi huo mkubwa wa kufua umeme, Els weldey na Arab Contructors, zinafanya kazi nzuri kwa hiyo zitatekeleza mradi huo kwa weledi mkubwa.

Umeme utakaozalishwa hapo unatarajiwa kusafirishwa kutoka Rufiji kwenda Chalinze, kote katika mkoa wa Pwani, umbali wa kilomita 127 na kisha kutoka Chalinze unapelekwa mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma, ambako kutakuwapo vituo vikuu vya kusambaza umeme wa kuendesha treni ya kisasa (SGR).

> **Eneo la Selou ni eneo kubwa ambalo linachukua takribani kilomita 50, hivyo ni lazima Wizara igawanye eneo na kuanzisha hifadhi ya Taifa ili kukidhi mahitaji ya utalii na kukisaidia kizazi kijacho kuendelea kuenzi mambo ambayo ameyafanya baba wa Taifa**

## WENYE ENEO

Akizungumza katika mkutano wa kujadili namna ya kuilinda hifadhi hiyo mpya, Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhandisi Evarist Ndikilo, anasema ulinzi wa hifadhi hiyo ni jukumu la wananchi wote, chini ya viongozi wao wa wilaya na mikoa inayozunguka.

"Licha ya hifadhi hii kuwa kubwa kuliko zote, ndani yake kuna mradi mkubwa wa kufua umeme wa Nyerere, hivyo sote tuna jukumu la kuhakikisha hifadhi hii inalindwa na kuendelea kuwapo kwa maslahi ya vizazi vijavyo," anasema Ndikilo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, anashauri kwa kumuunga mkono Mhandisi Ndikilo, kuwa mikoa yote inayozunguka hifadhi, inapaswa kujipanga vizuri kuimarisha ulinzi na usalama katika hifadhi hiyo, kwani itakuwa na mchango mkubwa katika utalii hasa kwa Ukanda wa Kusini, ambao sada unahamasishwa zaidi.

Kamishina wa Uhifadhi kutoka Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Nchini (TANAPA) Dk. Allan Kijazi, anasema mamlaka hiyo tayari imeshaweka mikakati madhubuti katika hifadhi hiyo kutokana na sifa za pekee.

Anasema sifa moja ni kuitwa jina la mwanzilishi wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, pia uwapo wa mradi mkubwa wa umeme wa Nyerere.

Kamishna wa Uhifadhi kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) Dk. James Wambara, amehakikisha watakuwa na ushirikiano wa kutosha na wenzao wa TANAPA, kwa ajili ya kuilinda hifadhi hiyo kwa kuwa kanuni za uhifadhi ni zilezile.

## WASIFU WA HIFADHI

Hifadhi ya Taifa ya Nyerere inatambuliwa kuwa ndiyo hifadhi ya taifa kubwa kuliko yote nchini Tanzania, pia duniani kote.

Hifadhi ilianzishwa mwaka jana, kabla ya kupandishwa hadhi Lilikuwa pori tengefu lililojulikana kwa jina la Selous.

Hifadhi ya Nyerere inatajwa kuna na ukubwa linganishi, kushinda nchi 70 duniani, ikikadiliwa kuwa na eneo sawa na nchi za Kostarika (Marekani ya Kati na takribani mara mbili kuliko nchi ya Ubelgiji iliyopo Ulaya.

Sehemu kubwa ya eneo iko katika hali ya asili bila kuvurugwa na shughuli za binadamu. Mwaka 1982 iliorodheshwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi, Eloimu na Utamaduni (UNESCO) kuwa urithi wa dunia. Ilipofika mwaka 2014 iliingizwa katika orodha ya UNESCO kuwa hifadhi zenye hatari ya kupotea.

Jina la awali lilitokana na raia wa Uingereza Frederick Selous aliyekuwa mwindaji wakati ukoloni.

## WANYAMA WANAOPATIKANA

Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ina aina kadhaa za wanyamapori wanaopatikana ndani yake, kati yao wapo simba, nyumbu, twiga, pundamilia, kiboko, kifaru, swala, fisi, mbwa mwitu na idadi kubwa ya mamba na viboko wanaopatikana katika Mto Rufiji.

Hapo awali hifadhi ya Taifa ya Nyerere ilisifika kuwa tembo wengi lakini kwa sababu ya ujangili uliokithiri idadi imepungua sana.



Wanyama wakiwa ndani ya Hifadhi ya Nyerere, zamani. **PICHA: MTANDAO**



Mto unaopeleka maji, katika Bwawa na Umeme la Nyerere.





# Kanisa lakumbusha mema ya Magufuli

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

KATIBU Mkuu Msaidizi wa Kanisa la The Gospel Special Message Tanzania (GOME), Emmanuel Msengi, amesema Watanzania hawatamsahau Hayati Rais John Magufuli kutokana na kuwafikishia huduma za umeme, maji, barabara vituo vya afya na zahanati vijijini ambavyo toka uhuru hazikuwafikia.

Amesema Rais Magufuli hatasahaulika kwa Watanzania kutokana na maono yake ya kuanzisha miradi mikubwa ili kuhakikisha nchi inapiga hatua kubwa kwa ajili ya maendeleo yake kwa kutumia rasilimali zilizopo nchini.

Katibu Msengi aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu kifo cha Dk. Magufuli kilichotokea Machi 17, mwaka huu, mkoani Dar es Salaam.

Alisema vijiji vingi nchini toka nchi ipate uhuru havikuwahi kuona huduma za umeme, maji salama, barabara na vituo vya afya, lakini Hayati Dk. Magufuli alifanikisha kupata maendeleo hayo.

Alisema Dk. Magufuli aliwakomboa wananchi hao wa vijijini kwenye huduma hizo huku akiwa na maono makubwa ya kuanzisha miradi mikubwa ambayo itakayowaondolea Watanzania umaskini na kuwawezesha kukua kiuchumi.

"Pia tutamkumbuka kwa hili la matumizi mazuri ya fedha, nalo limekuwa na nidhamu ya hali ya juu, hili lilikwenda sambamba na kumtaka kila Mtanzania kumtaka kufanya kazi kwa bidii tofauti na huko nyuma ambako watu walikuwa wakishinda vijiweni na maisha ya ubaishaji," alisema.

Msengi aliwaomba watumishi wa Mungu kuibeba awamu ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyokabidhiwa kwa kuiombea ili nchi iendelee kuwa na amani na kuombea miradi yote iliyoanzisha, ikamilike na kutimiza ndoto za Dk. Magufuli.

"Tukumbuke kuwa siyo wote wanaopenda amani yetu hii tuliyopewa na kutunukiwa na Mungu na siyo kila mtu anayependa maendeleo yetu. Tunatakiwa watumishi kuomba ili roho hizo zisipate nafasi ya kuhujumu mafanikio yetu haya," alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa kwa maana hiyo, Watanzania kwa pamoja wanatakiwa kushirikiana katika maombi hayo kwa ajili ya kumbeba Rais na viongozi wanaomsaidia kwenye utendaji wake.




Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Erasto Sima, akitia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Dk. John Magufuli kwenye ofisi za makao makuu ya chama hicho, jijini Dodoma juzi. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

## ...Viongozi wa dini wamsifu kuwa daraja la maendeleo

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

VIONGOZI wa dini mkoani Dodoma, wamesema Rais John Magufuli alikuwa daraja lililokuwa likitumiwa na Watanzania kwa ajili ya kujipatia maendeleo na sasa limekatika.

Askofu Mkuu wa Makanisa ya Philadelphia Gospel Assembly Tanzania na nchi za Afrika ya Mashariki, Dk. Yohana Masinga, alisema jana kuwa Hayati Rais Magufuli ni kiongozi aliyekuwa amewawekea malengo ya maendeleo wananchi wake kutokana na kutanguliza maslahi kwa wananchi hususani wenye kipato cha chini.

Dk. Masinga aliwaomba viongozi walioko madarakani na Watanzania, kuendeleza kuenzi yale yote aliyokuwa ameyafanya kwa ajili ya maendeleo ya taifa huku wakiendelea kuombea amani na utulivu.

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alisema mafanikio ya miaka mitano ya uongozi wa Dk. John Magufuli yalitokana na kumcha Mungu kwa uaminifu na ndicho kinachopaswa kufanywa na viongozi waliopo kwenye madaraka kufuata nyayo hizo za kiutendaji.

Shekhe Rajabu alisema kuwa Rais Magufuli alimtanguliza Mungu kwa kila jambo na ndiyo maana alifanikiwa kwa vitendo ikiwamo watumishi wake kuwa na nidhamu ya hali ya juu kazini.

Aliwataka Watanzania kwenye kipindi hiki cha majonzi kuwa wavumilivu na kuondokana na tofauti ya aina yoyote na kuyaishi mazuri ya Hayati Dk. Magufuli.

Makamu Katibu Mkuu Taifa Kanisa la PHAM (T), Julias Bundala, alisema kifo cha kiongozi huyo ni pigo kwa Watanzania kutokana na utendaji wake wa kazi alivyokuwa akiwajali wananchi wake wa hali ya chini na huku akitimiza maono yake ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda.

## UDOM wasema watamkumbuka kwa mikopo

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wamesema watamkumbuka Hayati Rais Dk. John Magufuli kutokana na kuwasaidia kupata mikopo ya elimu ya juu na kusaidia kuondoa maandamano na migomo iliyokuwa inajitokeza awali.

"Suala la mikopo ilikuwa ni sehemu mojawapo ya kuchangia migogoro kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini iliyokuwa ikotokea mara kwa mara katika baadhi ya vyuo vikuu," mmoja wa mawaziri wa serikali ya wanafunzi wa UDOM, James Mwaijambe, alisema katika mazungumzo na Nipashe jana jijini hapa.

"Mkopo kwa mwanafunzi ni muhimu sana kwa sababu unasaidia kuendesha maisha yake anapokuwa masomoni," alifafanua.

Alisema bila mkopo, wanafunzi wengi hawawezi kumudu gharama za masomo ya elimu ya juu na watakwama kufanya mambo mengi ya msingi wakiwa chuoni.

Godfrey Ipyana, mwanafunzi wa UDOM, alisema Hayati Rais Magufuli alikuwa mwenye misimamo ambayo imesaidia kuifikisha Tanzania ilipo kwa sasa kimaendeleo.

Alisema kuwa Rais Magufuli alikuwa na uzalendo wa hali ya juu wa kupigania nchi yake na Watanzania kwa ujumla jambo ambalo limesababisha kufanya vitu vingi vya maendeleo ambavyo vinaonekana machoni kwa watu.

"Tuna kila sababu ya kumkumbuka Hayati Dk. Magufuli, ndiye aliyefanya elimu bure, ameboresha sekta ya afya pamoja na kupiga vita rushwa," alisema Ipyana.

Alisema vijana wanapaswa kuiga mfano wa Hayati Rais Magufuli, ili kulipeleka mbele taifa kimaendeleo.

Mwanafunzi huyo alisema Hayati Rais Magufuli alifanya hivyo ili kulifanya taifa kujitegemea badala ya kutegemea misaada.

Mwanafunzi Edna Ngoli alisema Hayati Dk. Magufuli alipiga vita rushwa ambayo imekuwa kikwazo kikubwa katika vyuo vya elimu ya juu na sehemu nyingine.

Alisema vijana wataendelea kumkumbuka Hayati Rais Magufuli kutokana na mambo makubwa ambayo ameyafanya kwa wanafunzi hususan kuwasaidia katika upatikanaji wa mikopo.

Alisema wanafunzi wa vyuo wataendelea kumlilia Dk. Magufuli kutokana na jinsi alivyojitoa katika utekelezaji wake wa maendeleo hususani kwenye suala la elimu.



# Kyela kumkumbuka JPM uboreshaji miundombinu

**Na Grace Mwakalinga, KYELA**

WAKATI mamia ya Watanzania wakiomboleza kifo cha Hayati Dk. John Magufuli, wananchi katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wamesema wataendelea kumkumbuka kwa kuwaletea maendeleo ikiwamo uboreshaji wa miundombinu wa vituo mbalimbali vya afya na ujenzi wa barabara kutoka Tenenda hadi Matema Beach kwa kiwango cha lami.

Walisema hayo wakati wa ibada maalum ya kumwombea Hayati Magufuli ambayo ilifanyika kwenye viwanja vya John Mwakangale.

Miongoni mwa wananchi hao, Anganile Amani, mkazi wa Mtaa wa Mikoroshini, alisema miongoni mwa alama alizoziacha Dk. Magufuli ni kujenga barabara ya lami yenye urefu wa kilomita zaidi ya 30 kutoka eneo la Tenende hadi Matema Beach ambayo ilikuwa ni vikwazo kwa wananchi wa Mwaya, Ipinda, Mababu, Ngyekye, Makwale, Ipande na Ikombe.

"Kifo cha Dk. Magufuli ni pigo kubwa kwetu wananchi wanyonge maana alisimama na sisi kwa kuhakikisha hatunyanyasiki na kupewa huduma kama wanavyofanyiwa matajiri, tuliishi kwa amani kwa kuwa tulijua mtetezi wetu yupo tunamwombea Mungu ampe pumziko la milele," alisema Amani.

Baadhi ya viongozi wa dini akiwamo, Askofu wa Kanisa la Anglikana, Joseph Mwambungu, alisema taifa limepoteza mtu muhimu ambaye mchango wake bado ulikuwa unahitajika kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi.

Aliwaomba Watanzania kuendelea kushikamana na kumtanguliza Mungu katika mambo yote huku wakiendelea kumuunga mkono, Rais Samia Suluhu Hassan ili kufika kwenye Tanzania inayotakiwa.

Kaimu Katibu Mtendaji Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe, Gabriel Kalinga, alisema wanaimani na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuyaendeleza mazuri yote yaliyoasisiwa na Hayati Dk. Magufuli kwenye nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

Mwakilishi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Kyela, Padri Julius Mwaisela, alisema hayati alikuwa kama askari kwenye vita ambaye hakukubali kutetereka na maeneo ya watu bali aliendelea kuchapa kazi.

Alisema dhamira ya kuwatumikia wananchi aliitimiza kwa vitendo kwa kuwa alisimamia misingi ya uwajibikaji na kuziba mianya ya rushwa na kuhimiza matumizi bora ya rasilimali za umma ili wananchi kunufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo. Shekhe Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Nuru Mwafula, alisema waumini wa kiislamu na wasio waumini wa dini hiyo kwa pamoja waendelee kumwombea Hayati Magufuli kupumzika kwa amani.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, aliwaomba Wanakyela kusimama imara na kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo.



Wakazi wa wilayani Kyela, mkoani Mbeya, wakiwa kwenye maombi maalum ya kumwombea Hayati Dk. John Magufuli kwenye Uwanja wa John Mwakangale, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# ...Wasomi vyuoni wasema kaacha mazingira mazuri elimu

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

VIJANA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wanaosoma kwenye vyuo vya kati na vikuu mkoani Mbeya wamesema watakumbuka uongozi wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli kwa vile umeacha katika sekta ya elimu kwa kuweka mazingira mazuri ya kitaaluma vyuoni.

Waliyasema hayo jana wakizungumza na waandishi wa habari walidai kuwa uongozi wa Hayati Dk. Magufuli umeacha alama kwenye sekta ya elimu kwa sababu alisimamia na kuhakikisha miundombinu ya elimu inaboreshwa pamoja na kupatiwa mikopo kwa wakati.

Mwenyekiti wa vijana wa CCM vyuo vya kati na vikuu, Halima Magumba, alisema Hayati Dk. Magufuli, alisaidia kuboresha mazingira ya elimu kwa vyuo vya kati na vikuu na kuhakikisha vijana wanaandaliwa ipasavyo kuwa wazalendo wa kulitumikia taifa na kujiajiri.

"Uongozi wa Hayati Magufuli umeacha alama kwenye sekta ya elimu nchini, ameboresha miundombinu ya elimu vyuoni, mikopo hata kwa wakufunzi wetu aliboresha makazi yao, sio tu vyuoni bali hata kwenye elimu ya msingi na sekondari alianzisha elimu bure hakika tumepata pigo kubwa," alisema Magumba.

Baadhi ya wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Erick Mgishagwe, aliwaomba viongozi kuendelea kuwa wazalendo kwa kuhakikisha wanasimamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aliwashauri viongozi kukumbuka maagizo ya Hayati Dk. Magufuli aliyoyatoa kuhusu kusimamia miradi mbalimbali ya wananchi na kuwachukulia hatua wala rushwa.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Ndaki ya Mbeya, Robert Magambo, alisema jukumu la kuijenga Tanzania mpya ni la kila Mtanzania na kutaka wananchi na viongozi waendelee kuijenga nchini.

## 'Imani potofu chanzo uharibifu mazingira'

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

IMANI potofu miongoni mwa jamii za wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, zimetajwa kuwa ndiyo chanzo cha uharibifu wa mazingira ikiwamo uchomaji ovyo wa misitu hali inayoathiri maisha ya viumbe hai.

Chifu wa kabila la Wasafwa, Roketi Mwashinga, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na mwandishi wa habari hizi kuwa ni wajibu kwa viongozi wa kimila kupambana na uharibifu wa mazingira na kuwakumbusha wananchi kuzingatia mipango miji.

Alisema imani potofu ambazo zinaaminisha watu kuwa baadhi ya uoto ni utajiri umechangia kwa kiasi kikubwa kupoteza uoto wa asili na kusababisha jangwa au ukame na kusababisha wananchi kuvamia makazi ya watu.

"Laiti machifu au wazee wa kimila wangekata miti ovyo au kuharibu maliasili kizazi cha sasa kisingenufaika na uoto wowote wa asili na huenda kungekuwa ni jangwa ndio maana tumeamua kulivalia njuga ili kuhakikisha hakuna uharibifu wa mazingira," alisema Mwashinga.

Alisema zipo baadhi ya imani kuwa kuchoma misitu kunasaidia kupata mazao mengi mashambani pamoja na kuwakamata kirahisi wanyama wa porini kwa ajili ya kitoweo na kwamba imani hizo zinaharibu ikolojia.

Alisema imani za aina hiyo ni za uongo na hazina faida yoyote kwa binadamu zaidi ya kuharibu mazingira ambayo ndiyo makazi ya viumbe hai mbalimbali wakiwamo wanyamapori, mimea mbalimbali, ndege pamoja na wadudu ambao wanapendezesha mazingira.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Stephen Katemba, alisema elimu ya utunzaji wa mazingira na kuzingatia miongozi inayohamasisha masuala ya mipango miji ambayo inatolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imesaidia kupunguza tatizo la uharibifu wa mazingira wilayani humo.

Alisema kwa sasa wamefanikiwa kudhibiti vitendo vya uchomaji misitu ovyo na kwamba wananchi wameanza kuelewa madhara ya matukio hayo na wanahamasishana wao wenyewe kulinda misitu.

Alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la upandaji miti jambo ambalo limesaidia utunzaji wa kimazingira na wanategemea elimu hiyo itasaidia kuifanya wilaya hiyo kuwa kinara utunzaji mazingira nchini.

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo, walisema kutokana na elimu waliyoipata ya utunzaji wa mazingira, watahakikisha wanalinda mazingira hasa misitu ili waondokane na matatizo ambayo yamekuwa yakiwakabili ikiwamo ukosefu wa maji.





# ZURA, ZRB kudhibiti vituo vya mafuta

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imesema inashirikiana na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kuhakikisha vituo vyote vya mafuta vinakuwa na mashine za kutolea risiti za elektroniki.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa mamlaka hiyo, Mbarak Hassan Haji, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema ZURA imeshaanza mazungumzo na bodi hiyo ili utaratibu huo kutumika katika vituo vya kuuzia mafuta.

"Katika suala hili ilikuwa haijaweka wazi moja kwa moja kuwa ni hiari au ni lazima mashine yako iwe ya kutoa risiti moja kwa moja na tumeanza kuwashauri na kuwaelekeza wafanye hivyo, lakini tutakapobadilisha kanuni na kuwa moja kwa moja ni sharti la lazima atakayejenga kituo atalazimika kuwa na mashine za mfumo wa kielektroniki," alisema.

Alisema kanuni hizo zitakapokamilika ZURA itatoa muda kwa vituo vya mafuta vya zamani hasa vinavyobadilisha mashine kutokana na hitilafu ili kubadilisha mashine hizo na ziweze kuendana na mfumo wa kielektroniki.

Aibainisha kwa sasa kuna kituo kimoja tu cha kuuzia mafuta huko kisiwani Pemba chenye mashine za mfumo wa kielektroniki.

"Tunaamini sio suala geni au lina gharama kubwa kwamba wamiliki wa vituo vya mafuta watashindwa kufanya, kitu hiki kinawezekana na tunakitengenezea mazingira mazuri kwani tukumbuke ZURA ipo kwa ajili ya kuwalinda wateja wake wote, ambao wanafanya kazi ikiwamo serikali kuhakikisha sera zake, mipango na maagizo yake yanafanyiwa kazi na mtoa huduma maslahi yake," alisema.

Kuhusu suala la risiti za kawaida zinazotolewa katika vituo vya mafuta ambazo hazionyeshi jina la kampuni hilo ni tatizo, ZURA italifuatilia jambo hilo ili kila kampuni inaweka jina lake katika risiti.

"Jambo hili sio tu katika risiti za mafuta pekee, hata risiti tunazopatiwa madukani hazionyeshi majina, hivyo ni kosa kwani zinatakiwa zionyeshe jina halisi ya sehemu unayopatiwa huduma ili unapopata tatizo uweze kutatuliwa kwa haraka," alisema.

Hivyo aliwasisitiza wananchi kufahamu umuhimu wa kudai risiti na kulichukua kwa msisitizo suala hilo na watakapopata hitilafu ya chombo ZURA itataka kielelezo pekee ambacho ni risiti, ambayo uliwekea mafuta katika kituo husika.

"Ukija kulalamika hapa kwamba chombo chako kimepata hitilafu kwa kuwekewa mafuta na kituo uje na uthibitisho ambao utaonyesha ushahidi hasa risiti ndio tutaweza kukusaidia kwa maelezo matupu hatutokubali na hutopata haki yako," alisisitiza.

Aliiomba ZRB kuongeza nguvu katika vituo vya mafuta ili kuhakikisha wanawapatia mashine hizo na kupunguza muda wa kutumia risiti za mkono.

Meneja Uhusiano Huduma kwa Walipa Kodi kutoka ZRB, Shaban Yahya Ramadhan, alisema bodi hiyo ipo katika mchakato wa kumtafuta msambazaji wa mashine za kielektroniki ili kuuza mashine za VFD ikiwamo kwenye vituo vya mafuta madukani na sehemu zote ambazo watu wanafanya miamala ya kibiashara.

Alisema ZRB itatoa zabuni kwa ajili ya kutafuta msambazaji huyo ili kuuza mashine hizo kwa wafanyabiashara na kuzuia mianya ya upotevu wa mapato ya serikali.

## Mawakala wa vyama uchaguzi mdogo wafundwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAWAKALA wa vyama vya siasa watakaoshiriki uchaguzi mdogo wa Jimbo la Pandani na Wadi ya Kinuni unaotarajiwa kufanyika Machi, 28 mwaka huu, wametakiwa kufuata sheria na miongozo watakayopatiwa na wasimamizi wa uchaguzi.

Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imesema malengo ni kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi katika vituo vya kupigia kura.

Mkuu wa Kurugenzi ya Huduma za Uchaguzi wa ZEC, Khamis Issa Khamis, aliyasema hayo wakati, akifungua mafunzo ya mawakala wa uchaguzi wa Wadi ya Kinuni yaliyofanyika Shule ya Sekondari ya Abeid Amani Karume iliyopo Kinuni.

Khamis alisema, katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Pandani na Wadi ya Kinuni Tume itatumia sheria na kanuni zilizotumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, hivyo ni vyema mawakala wanaowakilisha vyama katika vituo wakatulia na kuendelea kuilinda amani.

Naye Ofisa Uchaguzi Wilaya ya Kati, Said Ramadhani Mgeni, wakati akiwasilisha mada katika mafunzo hayo, alisema kila chama cha siasa kina haki ya kuteua wakala mmoja kwa kila kituo, ambaye atatoka katika eneo la kupigia kura, wakala wa upigaji kura, kuhesabu au kujumlisha kura.

Mafunzo ya siku moja ya mawakala wa vyama vya siasa katika vituo vya kupigia kura yalifanyika Unguja na Pemba yakiwa ni matayarisho ya uchaguzi mdogo wa Jimbo la Pandani na Wadi ya Kinuni unaotarajiwa kufanyika Machi, 28, baada ya wateule wa wadi na jimbo hilo kufariki dunia.

**Khamis alisema, katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Pandani na Wadi ya Kinuni Tume itatumia sheria na kanuni zilizotumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, hivyo ni vyema mawakala wanaowakilisha vyama katika vituo wakatulia na kuendelea kuilinda amani.**



Mtaa maarufu wa Gizenga, jijini Zanzibar wenye msongamano wa watu, ukiwa kimya huku maduka yakiwa yamefungwa mapema wiki hii, baada ya wafanyabiashara wote kwenda Uwanja wa Amaan, kumuaga aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Hayati Dk. John Magufuli. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## ZPPDA yashtukia uadilifu kwenye biashara kushuka

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAMLAKA ya Manunuzi na Uondoaji Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA), imesema pamoja na serikali kuweka mazingira bora kwa wafanyabiashara, lakini bado kumekuwapo na kupungua kwa uadilifu wa kibiashara hasa wanapouza bidhaa serikalini.

Mkurugenzi Idara ya Ukaguzi, Uchunguzi na Ufuatiliaji, Mohammed Omar Mmoka, aliyasema hayo katika mkutano uliowashirikisha wafanyabiashara wenye lengo la kupata maoni yao juu ya marekebisho ya sheria ya manunuzi uliofanyika katika ofisi zao Mazizini.

Alisema taasisi za serikali mara nyingi hufanyiwa mauzo kwa bei kinyume na uhalisia hali inayoharibu thamani ya biashara Zanzibar. Aidha, alisema kuwa lengo la serikali ni kuona wanakuza mitaji ya wafanyabiashara na sio jambo jingine.

Hata hivyo, alisema kushuka kwa maadili ya kibiashara yanasababisha kutokea malalamiko kwa wananchi juu ya bei kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Mkurugenzi huyo alisema hata sehemu ya utekelezaji wa miradi ya serikali ikiwamo ujenzi wa barabara hujengwa kwa kutofikia viwango vinavyotakiwa na kuitia hasara serikali kurejea ujenzi kwa mara nyingine.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Chama cha Wafanyabiashara Zanzibar, Hamad Hamad, alisema ipo haja kwa mamlaka hiyo kutoa mafunzo kwa wadau wake ili kuona kuna fursa sawa pamoja na uwazi katika masuala ya manunuzi.

Alisema elimu waliyopewa yanaonyesha matumaini ya kuwapo uwazi katika masuala ya kibiashara pale serikali inapopata tenda wanakwenda wao kama wazawa, lakini hawapewi tenda hizo na badala yake huchukua kampuni za nje ingawa wanajenga kwa gharama kubwa.

Wafanyabiashara walioshiriki mkutano huo walisema chanzo cha kushuka maadili ya biashara ni wafanyakazi wa serikalini kutokuwa waadilifu katika kutekeleza majukumu yao hasa katika suala la manunuzi.

Walisema pamoja na kutokuwa na uaminifu kati ya wafanyabiashara, lakini wafanyakazi wanafahamu bei za manunuzi wanayofanya, lakini wamekuwa wakikubali kufanya manunuzi ya vitu visivyoendana na thamani kwa malengo wanayoyafahamu wenyewe. Juma Burhan, mmoja wa wafanyabiashara hao, alisema zimewekwa kodi kubwa, hivyo kusababisha bei kupanda.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**katika Mahakama ya Mwanzo CHAMWINO MJINI**
**Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**SHAURI LA NDOA NA. 16/2021**
**SHANI JUMA MHANDO……….......MDAI**
**RIZIKI TARAMO MAJURA…………………………..MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)
KWA: RIZIKI TARAMO MAJURA
WA MKOA WA SONGWE KIJIJI CHA NGWARA
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
MADAI YA TALAKA NA MGAWANYO WA MALI
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 mwezi 3 mwaka 2021 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 mwezi 3 mwaka 2021.

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**IBRAHIM OMARY CHIVI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina la **CHARLES SAIMON MAMBA** aina ya BOXER yenye namba za usajili **MC 622 BYJ.Chassis No.MD2B15BY3JWM88715, Engine No.JVZWJM19051** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/63011/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**
**MAOMBI NA. 45 YA 2021**
**ABRAHAMU TERRY MJEMA………MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1.BENEDICT JOSEPH**
**2.PETER REUBENI RITE……….WAJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**PETER REUBENI RITE**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 08/04/2021 mbele ya Mh.E.Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukuosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautohudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 23 mwezi march 2021.

**E.Mogasa**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 58 LA 2021**
**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya marehemu**
**SHADRACK E.R.Z NLIGA**
**MWOMBAJI**
**JULIANA RONALD NLIGA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**Kanuni 75**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hii katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 19 mwezi wa 4 mwaka 2021
Hati hii imetolewa 25 mwezi 3 mwaka 2021

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

**IN THE DISTRICT COURT OF MOSHI**
**AT MOSHI**
**CIVIL CASE NO.19 OF 2020**
**FELISTA KINANA CHUWA……………..........1ST PLAINTIFF&ANOTHER**
**VERSUS**
**1)OSCAR LUCAS KIMARO…………………………….......………1ST DEFENDANT**
**2)DIDAS RAPHAEL KARIA……………............2ND DEFENDANT**
**3)THE HERITAGE INSURANCE COMP.LTD……….............………………3RD PARTY**

**NOTICE OF MENTION/HEARING**
TO: OSCAR LUCAS KIMARO(1st DEFENDANT)
Take Notice that the above case has been fixed for mention in the District Court of Moshi at 1st the day of April 2021.
You are hereby ordered to appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day any document under which you intend to rely in support of your case.
TAKE FURTHER NOTICE that, default of your appearance on that day afore mentioned the court will proceed with the matter in your absence.
Given under my hand and seal of this Court this 12th day of March, 2021

**PRINCIPAL**
**RESIDENT MAGISTRATE**
**MOSHI**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

TOTAL FISCAL SOLUTIONS LTD INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 807 BPR TOYOTA PROBOX. CHASSIS NAMBA NCP58-0038265. ENGINE NAMBA INZ-FEB495163. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: DAR/URA/RB/164741/2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**
**MAOMBI NA. 45 YA 2021**
**ABRAHAMU TERRY MJEMA………………MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1.BENEDICT JOSEPH**
**2.PETER REUBENI RITE……………………..WAJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**PETER REUBENI RITE**
Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 08/04/2021 mbele ya Mh.E.Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukuosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautohudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 23 mwezi march 2021.

**E.Mogasa**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

## TANGAZO LA NOTISI KULIPA DENI

TUJIJENGE TANZANIA LTD tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku Thelathini(30) kuanzia tarehe ya tangazo hili, vinginevyo tutalazimika kuchukua hatua zaidi za kisheria ikiwemo kuwaruhusu madalali kukamata nakuuza kwa njia ya mnada wa hadhara.

1. Amina Abubakar Swedi- MC.474 AKX, TVS KING
2. Nuhu .A. Sansa - T.402 CQB, Nissan Civilian
3. Catherine Albert Mshatta- T.162 DEE, Toyota Raum
4. Justin Leornad Twahilwa- T.420 BRM, Toyota Vitz
5. Mathew Aidan Ngonyani- T.592 CFK,Toyota Corona Premio
6. Nictagon Amon Itege - T.122 DEM, Toyota Vitz
7. Saul Kibutu Aswile - T.954 DFX, Toyota Sienta
8. Seth P Sekao - T.297 DEF, Daf Trucks
9. Shina Rehege/ Mwajuma Jibadi Mwanuke – T.868 ASM, SCANIA; T.109 CHE, VOLVO
10. Zainab Shabani Kakoso- T.998 DFY, Toyota Isis

**Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0718068335 au**
**Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA. 207/2020**
**REUBEN MARTIN ...................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JUDITH NGAIZA**
**BELENADO VALISTA ..................WAJIBU MAOMBI**
**KWA: JUDITH NGAIZA**
**BELENADO VALISTA**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/unaarifiwa kuwa Maombi Na. 207/2020 yamepangwa kutajwa tarehe 21/04/2021 mbele ya mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.
Hivyo, munaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/ mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 17/03/2021.

……………………………………………
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**BUKOBA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.**
**WILAYA YA MOSHI**
**MAOMBI NA. 174/2020**
**EDITHA LUKA MASSAWE……....MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**PANCRAS LUKA MASSAWE**
**FINCA MICROFINANCE BANK LTD…....WAJIBU MAOMBI**
**LOCUS DEBT MANAGEMENT LTD**
**KUITWA SHAURINI**
**KWA : LOCUS DEBT MANAGEMENT LTD**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mleta maombi ameleta maombi ya kesi na ameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 29/03/2021 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti P.J.Makwandi hivyo unatakiwa kufika mahakamani wewe au wakili wako.
ANGALIA: Kama hautahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakamani itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Barza hili leo tarehe 18 mwezi, Machi ,2021.

……………………………………………
**P.J.Makwandi**
**MWENYEKITI.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaomba NATO kuungana dhidi ya China

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Anthony Blinken, alijizuia kutoa maneno makali ya kuikosoa China na badala yake ametoa wito kwa washirika wake kuungana na Marekani.

Katika hotuba yake ya ufunguzi katika siku ya pili ya mkutano na washirika wa Jumuiya ya Kujihami (NATO) aliyoitoa juzi, Blinken, amegusia masuala yahusuyo uhusiano wa nchi hiyo na washirika wake, vitisho vya Urusi hadi China pamoja na matatizo ya kiulimwengu.

Blinken, alirudia msimamo wa Marekani wa kuiunga mkono NATO, akisema nchi hiyo imejitolea kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kutekeleza kifungu cha 5, kinachoelezea wajibu wa kuhakikisha ulinzi miongoni mwa wanachama.

Lakini, serikali kadhaa za Marekani zilizopita zilisisitiza kuhusu michango, zikiwataka wanachama wengine wa NATO kuongeza mchango wa ulinzi kwenye jumuiya hiyo kwa asilimia 2 ya pato lao jumla la ndani.

Blinken pia, alihimiza kuyapa kipaumbele maamuzi yahusuyo vitisho vya kiulimwengu kama janga la COVID-19 na mabadiliko ya tabianchi.

Kwenye hotuba hiyo, alikosoa kile alichoita tabia ya uonevu ya China huku akiapa kuishinda.

Hata hivyo, amesema hiyo haimaanishi kwamba mataifa mengine hayapaswi kushirikiana na China pale inapopatikana, kwa mfano kwenye changamoto za mabadiliko ya tabianchi na usalama wa kiafya.

"Marekani haitawalazimisha washirika wetu kuchagua ama sisi au wao. Hakuna mjadala kuhusiana na mwenendo wa Beijing kwamba unatishia muungano wetu wa kiusalama pamoja na ustawi ni kwamba inafanya kila liwezekanalo kukiuka misingi ya mifumo ya kisheria ya kimataifa na maadili yetu.

"Lakini hiyo haimaanishi kwamba nchi haziwezi kushirikiana na China pale inapowezekana kwa mfano katika changamoto kama mabadiliko ya tabianchi na usalama wa kiafya."

Wasiwasi baina ya China Magharibi umeongezeka hivi karibuni baada ya Umoja wa Ulaya, Marekani, Canada na Uingereza kuwawekea vikwazo maofisa wa China na kampuni kutokana na madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu, hatua ambayo pia ilijibiwa na nchi hiyo kwa vikwazo.

Blinken pia aligusia tabia ya ubabe wa Urusi, akisema anadhani ni vyema wakaanzisha uhusiano na taifa hilo ambalo yanaweza kutabirika na endelevu.

Hata hivyo, alisema pamoja na hatua hiyo, bado hawatasita kuiwajibisha Urusi kutokana na hatua zake za ovyo na za ushindani ama uadui. Kabla ya hotuba hiyo, NATO ilikosoa vikali sera za ndani na za nje za Urusi.

DW



Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, akilihutubia Bunge jana, baada ya kuondoa vizuizi vya sikukuu ya Pasaka. **PICHA: REUTERS**

## Ujerumani yaruhusu watu kuchangamana Pasaka

**BERLIN,** UJERUMANI

KANSELA wa Ujerumani, Angela Merkel, amebadilisha uamuzi wake wa kuzuia shughuli za kiuchumi wakati wa sikukuu ya Pasaka, uliolenga kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona.

Duru zimeliambia Shirika la Habari la Kijerumani DPA kwamba hatua ya kubadili uamuzi huo, imechukuliwa baada ya kauli za kuukosoa kuongezeka.

Kansela Merkel ameueleza mkutano jana kwamba uamuzi wa mwanzo uliofikiwa mwanzoni mwa wiki hii wa kufunga maduka mengi zaidi Ujerumani na kupigwa marufuku mikusanyiko kwa siku tano kuanzia Aprili Mosi hautatekelezwa.

Kiongozi huyo wa Ujerumani amekiri kufanya kosa na kuomba radhi.

Tangazo hili jipya limesababisha mkanganyiko kuhusu mkakati wa serikali wa kupambana na janga la virusi hivyo.

DW

## UNHCR yaguswa ufungwaji kambi za wakimbizi Kenya

**GENEVA,** USWIZI

TUME ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), imesema itaendelea kushauriana na Kenya baada ya nchi hiyo kutangaza kufunga kambi mbili za wakimbizi ndani ya siku 14 zijazo kwa sababu za kiusalama.

Kambi hizo ni zile za Dadaab na Kakuma ambazo UNHCR imesema inaguswa na kutiwa wasiwasi na hatua hiyo ya serikali ya nchi hiyo kutaka kuzifunga katika kipindi hiki kigumu ambacho dunia inakabiliwa na janga la corona.

Hatua ya serikali imeshutumiwa na mashirika ya kiraia yakiongozwa na tume ya kutetea haki za binadamu.

Hii siyo mara ya kwanza kwa Kenya kutishia kufunga kambi hizo zinazowapa hifadhi wakimbizi zaidi ya laki nne, wengi wakiwa ni raia wa Somalia.

RFI

## Korea Kaskazini yarusha makombora Japan

**PYONGYANG,** KOREA KASKAZINI

KOREA Kaskazini imerusha makombora mawili kuelekea baharini nchini Japan, likiwa ni jaribio kubwa la kwanza kufanywa na serikali ya Pyongyang tangu kuingia madarakani kwa Rais wa Marekani, Joe Biden.

Korea Kaskazini imefanya majaribio ya makombora yake licha ya kuzuiwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kwa sababu ni hatari kwa usalama.

Japan ilisema kuwa hakuna mabaki ya makombora hayo, yamefika katika mipaka yake ya majini na hatua hiyo ya Korea Kaskazini inakuja siku chache baada ya kurusha makombora mengine mawili kuelekea Bahari ya Njano, inayopatikana kati ya China na eneo la Korea.

Waziri Mkuu wa Japan, Yoshihide Suga, alisema majaribio hayo ya Korea Kaskazini yanatishia usalama wa nchi hiyo na ukanda mzima, ambayo pia yamethibitishwa na Jeshi la Korea Kusini.

Rais wa Marekani, Biden, hajazungumzia majaribio haya ya hivi punde, lakini siku ya Jumanne, alisema jaribio la makombora ya masafa mafupi, lililotekelezwa na Korea Kaskazini, halikuwa tishio kwa Marekani.

RFI

## Shambulizi latikisa Palma

**MAPUTO,** MSUMBIJI

WATU wenye silaha wameshambulia mji wa Kaskazini mwa Msumbiji, Palma, wenye mradi wa gesi wa gharama za mabilioni ya dola unaoongozwa na kampuni kubwa ya mafuta ya Kifaransa, Total, vyanzo vimeeleza.

Uvamizi huo umefanyika wakati ilipotangazwa kuwa ujenzi utaanza hivi karibuni.

Kazi ilisimama mwezi Desemba kwa sababu za kiusalama zilizodaiwa kusababishwa na wanamgambo wa kiislamu Kaskazini mwa nchi hiyo, uasi ulioanza tangu mwaka 2017.

Milio ya risasi ilisikika mjini humo na kisha mawasiliano yalikatwa, Shirika la habari la Reuters lilinukuu vyanzo vya taarifa vikizungumza na shirika la habari la Kiren, Lusa.

Maelfu ya watu wamekimbia machafuko katika mji wa Cabo Delgado ulio Kaskazini mwa Msumbiji.

BBC



# DESCHAMPS AWALAUMU WACHEZAJI

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, amekilaumu kikosi chake kwa kukosa nguvu katika kipindi cha pili na kulazimishwa sare ya 1-1 dhidi ya Ukraine Jumatano, na kusema walitakiwa kumaliza mchezo huo kipindi cha kwanza.

Mabingwa hao watetezi wa Kombe la Dunia walianza safari yao ya kufuzu mashindano hayo nchini Qatar 2022 kwa staili isiyofurahisha jijini Paris, ingawa walionekana kwenye nafasi ya kuchukua pointi zote tatu kipindi cha kwanza.

Antoine Griezmann alifunga bao la kuongoza dakika ya 19 kabla ya Olivier Giroud kukosa nafasi kadhaa za wazi za kufunga.

Ukraine walisawazisha bao hilo dakika ya 57 kupitia kwa Presnel Kimpembe aliyejifunga baada ya kuligonga shuti la Serhiy Sydorchuk.

"Tulitakiwa tushinde mchezo ule kipindi cha kwanza, tulikuwa na nafasi nyingi, kipindi cha pili kilikuwa kigumu," alisema Deschamps akiiambia TF1 mara baada ya mchezo huo.

"Kulikuwa na uvivu kidogo, bao tulilolíruhusu liliweza kuepukika, na timu ilionekana kutokuwa kwenye kiwango bora.

"Tulikosa nguvu na ndio maana hatukuweza kuwa na matokeo tuliyoyataka, na hata kwenye ulinzi bado hatukuwa kwenye kiwango kizuri."

Ufaransa itacheza mchezo mwingine Jumapili dhidi ya Kazakhstan kabla ya Jumatano kucheza na Bosnia-Herzegovina.

## LOW AKANUSHA KUPATA KAZI LALIGA

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA Mkuu wa Ujerumani, Joachim Low amebainisha kwamba ana mpango wa kujifunza lugha ya Kihispania siku zijazo, lakini amesisitiza hana klabu ya kujiunga nayo kwenye LaLiga.

Low ataachana na kazi ya kuinoa Timu ya Taifa ya Ujerumani baada ya mashindano ya mataifa ya Ulaya kipindi cha majira ya joto baada ya Shirikisho la Soka la Ujerumani (DFB), kukubali maombi ya kujiweka pembeni.

Mkataba wake ulikuwa unamalizika baada ya michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2022, lakini badala yake Low ataachana na kikosi hicho baada ya mashindano hayo ya 2020 ambayo yataanza Juni mwaka huu.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 61 amekuwa kwenye nafasi hiyo tangu mwaka 2006 alipochukua mikoba ya Jurgen Klinsmann na kuiwezesha nchi hiyo kushinda Kombe la Dunia mwaka 2014.

Akizungumza na waandishi wa habari kabla ya michezo ya kufuzu michuano ya Kombe la Dunia dhidi ya Iceland, Romania na Macedonia, Low alikanusha kupata kazi katika nchini Hispania.

"Nilikuwa nafikiri hivyo muda mchache uliopita. Lakini sina klabu yoyote niliyokubaliana nayo kuinoa," alisema Low.

"Unaweza kutumia lugha ya Kihispania duniani kote. Amerika Kusini, Ulaya na Marekani unaweza kutumia lugha hii. Baada ya Kiingereza, hii ni lugha muhimu sana."



## BAYERN YAMFUNGIA KAZI VAZQUEZ

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich imeanza mazungumzo na winga wa Real Madrid, Lucas Vazquez ili kunasa saini yake kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Raia huyo wa Hispania mkataba wake wa sasa pale Madrid unamalizika mwishoni mwa msimu huu na hivyo Bayern wanaweza kumpata mchezaji huyo kwa uhamisho huru bila ada.

Kwa sasa Vazquez hana nafasi ya kuanza katika kikosi cha kwanza cha kocha Zinedine Zidane ambacho kina malengo makubwa ya kubeba ubingwa wa Laliga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wakati mkataba wa Vazquez unamalizika mwishoni mwa msimu huu, Real Madrid haijaonyesha nia ya kuendelea na huduma yake.

Gazeti la Bild la Ujerumani limeripoti kwamba, Bayern ipo kwenye nafasi ya kumnasa mchezaji huyo mwishoni mwa msimu huu ili kuimarisha kikosi chake.

Bayern ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwa sasa wapo kwenye harakati za kukisuka tena kikosi chake hicho, licha ya kusheheni mastaa kadhaa.

## HABARI MICHEZO



# UNITED
## YAJIPANGA KUMSAJILI LLORIS

**LONDON, England**

GOLIKIPA wa Tottenham Hotspur, Hugo Lloris, ameingia kwenye rada za kuwaniwa na Manchester United wakiwa na nia ya kumsajili kipindi cha majira ya joto, kwa mujibu wa L'Equipe.

United inamwona Lloris kama ndio chaguo sahihi la kuchukua nafasi ya David de Gea ambaye anatajwa kwamba, anataka kutimka kwenye kikosi hicho mwishoni mwa msimu huu.

De Gea ambaye katika misimu ya hivi karibuni amekuwa akifanya makosa mengi na kuigharimu timu, ameripotiwa kutokuwa na furaha kwenye kikosi hicho na sasa anataka kuondoka, baada ya kukaa kwa misimu 12.

Na United waliripotiwa wapo tayari kusikiliza ofa kwa De Gea huku kocha, Ole Gunnar Solskjaer akimtupia jicho Lloris.

Klabu ya Paris Saint-Germain ilikuwa mbele katika kuwania saini ya de Gea, huku kukiwa hakuna mazungumzo yaliyoripotiwa kufunguliwa hadi sasa baina ya klabu hizo mbili.

Lloris mwenye umri wa miaka 34 pia amepigiwa upatu kuondoka Spurs ili kwenda kutafuta changamoto mpya na hivyo, huenda safari yake ikaishia kule Old Trafford.

## BALE HAKUWA NA FURAHA SPURS – RAIS

**MADRID, Hispania**

RAIS wa zamani wa Real Madrid, Ramon Calderon, amesema mchezaji Gareth Bale hajafurahia kipindi chake akiwa kwa mkopo kule Tottenham Hotspur.

Bale ametangaza kurejea katika klabu yake ya Real Madrid pale mkataba wake wa mkopo katika klabu ya Tottenham utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu, kipindi cha majira ya joto.

Mchezaji huyo alijiunga na klabu hiyo mapema Septemba, mwaka jana baada ya kuwa na uhusiano mbaya na kocha wake, Zinedine Zidane pale katika dimba la Santiago Bernabeu.

Bale amecheza mechi 12 za Ligi Kuu England akiwa na Tottenham msimu huu tangu ajiunge nao, lakini sasa Calderon anaamini mchezaji huyo hana furaha chini ya Kocha Jose Mourinho.

"Ni wazi kwamba, Bale hakuwa na hana furaha kwa kipindi anachocheza Tottenahm," alisema Calderon akinukuliwa na gazeti la Marca.

"Bahati mbaya sio yeye tu wachezaji wote hawajawa na furaha chini ya kocha Jose Mourinho, hilo liko wazi kabisa," aliongeza kusema Calderon.




## SAINI YA KANE YAWINDWA MADRID

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid wamewaambia viongozi wa Tottenham kwamba, chaguo lao la kwanza kwenye usajili ni mshambuliaji wao Harry Kane ili ajiunge na kikosi hicho msimu ujao, kwa mujibu wa Sky Sport.

Miamba hao wa soka la Hispania wapo kwenye hesabu za kumsaka mshambuliaji daraja la kwanza pale msimu wa 2020/21 utakapomalizika na na wanaamini kwamba, Kane ni chaguo sahihi kwao ikiwa watapata saini yake.

Mbali na Kane pia inaelezwa kuwa Real Madrid wanavutiwa na uwezo wa mshambuliaji wa kikosi cha Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe na ikiwa watamkosa wataongeza nguvu kumsaka nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

Ripoti zimeeleza kuwa Real Madrid wanaamini kwamba makubaliano ya kumpata Kane ni rahisi kwao na yanawezekana tofauti na kupata saini ya Mbappe au Haaland.

Madrid chini ya Zinedine Zidane inahitaji kuboresha kikosi hicho huku wakiamini kwamba kumpata Kane ni rahisi zaidi.

Kane ambaye ni nyota ndani ya Tottenham inayonolewa na Jose Mourinho amecheza jumla ya mechi 377 na kufunga mabao 215 ndani ya misimu nane.

## HABARI MICHEZO

### KWA UFUPI

**SUAREZ KUREJEA LIVERPOOL**

LIVERPOOL imeweka wazi nia ya kumsajili tena fowadi wa Atletico Madrid na Uruguay, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 34. (**Fichajes via Four Four Two**)

**COSTA, BENFICA SAFI**

FOWADI wa zamani wa Atletico Madrid, Diego Costa mwenye umri wa miaka 32, atai-chezea Benfica msimu ujao baada ya kufikia makubaliano na klabu hiyo ya Ureno. (**Mundo Deportivo - in Spanish**)

**MADRID MASHAKANI**

RAIS wa zamani wa Real Madrid, Ramon Calderon ana mashaka kama klabu hiyo ina fedha za kutosha kumsajili straika wa Tottenham na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, wakati wa kipindi cha majira ya joto. (**Talksport**)

**DIAZ KURUDI MADRID**

REAL Madrid wanataka kumrudisha straika Brahim Diaz mwenye umri wa miaka 21, baada ya kumaliza muda wake wa kucheza kwa mkopo kule AC Milan. (**Calciomercato**)

**MADRID YAMCHUNIA RONALDO**

KLABU ya Real Madrid haijaonyesha nia ya kutaka kumrejesha mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36. (**COPE**)

**TORRES AITAMANI UNITED**

MLINZI wa Villarreal mwenye umri wa miaka 24, Pau Torres atapenda zaidi kujiunga na Manchester United kipindi cha majira ya joto. (**Manchester Evening News**)

**JOHNSTONE ANUKIA SPURS**

MLINZI wa zamani wa Tottenham Hotspur, Alan Hutton ameishauri klabu hiyo kumsajili golikipa wa England, Sam Johnstone kutoka West Brom ili kuchukua nafasi ya Hugo Lloris. (**Football Insider**)

**WRIGHT AMBEBA ODEGAARD**

STRAIKA wa zamani wa Arsenal, Ian Wright amesema klabu huyo inatakiwa kumsajili kwa mkataba wa kudumu kiungo wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, anayecheza hapo kwa mkopo kutoka Real Madrid. (**Ringer FC's Wrighty's House podcast via Metro**)

**SUNDERLAND SOKONI**

KLABU ya Sunderland imeanza mazungumzo na Wolves kwa ajili ya kumsajili moja kwa moja mlinzi, Dion Sanderson mwenye umri wa miaka 21 anayecheza hapo kwa mkopo ambaye ada yake ni pauni milioni mbili. (**Daily Mail**)

**GRIEZMANN HAONDOKI**

FOWADI wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30, anataka kubaki kujithibitishia ubora wake pale Barcelona. (**Radio Catalunya via AS**)

**PULISIC KUCHEZA OLIMPIKI**

WINGA wa Chelsea, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 22, amesema anataka kuiwakilisha Marekani kwenye michezo ya Olimpiki jijini Tokyo. (**NBC Sports via Evening Standard**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR KUSAINI MKATABA MPYA PSG

**Inaelezwa mazungumzo kati ya vigogo hao wa Ufaransa na wakala wake...**

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris St-Germain ipo kwenye mazungumzo na wakala wa nyota wake, Neymar kwa ajili ya kumwongezea mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo.

Neymar mwenye umri wa miaka 29 raia wa Brazil, majaliwa yake yamekuwa na mjadala mkubwa katika miezi ya hivi karibuni, lakini PSG wapo tayari kumpa mkataba mpya wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Kwa mujibu wa jarida la France Football, mazungumzo kati ya PSG na wakala wa Neymar yameelezwa kuwa yapo kwenye hatua nzuri na hakuna tena hofu ya mashabiki wa timu hiyo kumpoteza katika dirisha lijalo.

Hapo awali zilizagaa taarifa kuwa huenda Neymar akarejea tena Barcelona mwisho wa msimu huu.

Mkataba huyo mpya anaotarajiwa kusaini utamwongezea miaka minne zaidi kwenye mkataba wake wa sasa unaotarajiwa kumalizika mwaka 2022, hivyo akisaini atakaa na klabu hiyo hadi mwaka 2026.

Barca ilianza kuhusishwa kuhitaji saini ya Neymar tangu dirisha lililopita, huku wagombea wengi wa nafasi ya urais wa klabu hiyo walikuwa wakitoa ahadi kwamba wakichaguliwa watafanikisha mchakato kumrudisha nyota huyo.

Lakini tangu Joan Laporta achaguliwe kuiongoza timu hiyo nguvu kubwa amejiwezeka kwenye kupambana kuhakikisha Lionel Messi anaendelea kusalia klabuni hapo.

Hadi sasa Neymar amecheza mechi 18 za michuano yote na kufunga mabao 13.

HABARI MICHEZO

# NIYONZIMA AMFUNIKA MIQUISSONE AFCON

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Simba, Luis Miquissone akiwa na Timu ya Taifa ya Msumbiji, alishindwa kufurukuta na kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Rwanda (Amavubi), inayoongozwa na nahodha, Haruna Niyonzima anayeichezea Yanga ya hapa nchini.

Nyota mwingine wa Amavubi anayecheza soka la kulipwa nchini Tanzania ni Meddie Kagere wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba.

Amavubi iliondoka na pointi zote tatu katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) zinazotarajia kucheza mwakani nchini Cameroon.

Lilikuwa ni bao la dakika ya 70 lililofungwa na straika anayechezea timu ya APR ya Rwanda, Lague Byiringiro na kuifanya timu yake iliyoko katika Kundi F, kutoka mkiani hadi kwenye nafasi ya pili baada ya kufikisha pointi tano. Msumbiji inabaki kwenye nafasi ya tatu ikiwa na pointi nne.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Nyamirambo, ilikuwa na wachezaji watatu ambao wote wanacheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wachezaji hao wataendelea kusalia kwenye timu zao za tiafa hadi Machi 30, mwaka huu kwa ajili ya kushuka dimbani tena kwa ajili ya mechi nyingine za kuelekea AFCON.

Miquissone na timu yake ya Msumbiji watakuwa nyumbani kucheza dhidi ya Cape Verde wakati Niyonzima ambaye aliwahi pia kuichezea Simba na Kagere watakuwa ugenini kuwavaa Cameroon.

Baada ya mechi hizo, nyota hao watarejea nchini kujiunga na klabu zao kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika kwa upande wa wachezaji wa Simba.

Katika mechi hizo za kusaka tiketi ya kucheza AFCON, Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), yenyewe jana ilikuwa ugenini ikicheza dhidi ya Equatorial Guinea na Jumapili itawakaribisha Libya kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni, wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON-Beach Soccer), dhidi ya Burundi itakayochezwa Machi 30, mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Prisons yaipigia hesabu Yanga

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Tanzania Prisons umesema utaanza rasmi programu ya mazoezi hapo kesho baada ya kusimama kwa muda wa wiki ili kupisha maziko ya aliyekuwa Rais, Dk. John Pombe Magufuli.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaban Kazumba alisema mazoezi watakayoanza yataendelea kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kufanya vizuri katika mechi zilizobakia za Ligi Kuu Bara na Kombe la FA.

Kazumba alisema mechi zote zilizobakia zitakuwa na ushindani kwa sababu kila timu inahitaji kufikia malengo, na hivyo michezo yote itakuwa inafanana na fainali.

Aliongeza usajili ya kuboresha vikosi uliofanywa kwenye dirisha dogo la usajili umezaa matunda kwa timu zote baada ya kufahamu ilipokosea katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tutaendelea na mazoezi keshokutwa (kesho), huku tukiwa tunasubiri taarifa kutoka Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kama kutakuwa na mabadiliko yoyote ya kalenda ikiwamo mechi za FA au ligi".

"Kama ratiba itaendelea kubaki, vile vile nina imani tutaendelea kujiandaa na mchezo wetu wa FA dhidi ya Yanga kuhakikisha tunafanya vizuri katika hatua hiyo ya 16 bora," alisema Kazumba.

Mzunguko wa 25 wa Ligi Kuu Tanzania Bara unatarajiwa kuanza ifikapo Aprili 8, mwaka huu muda ambao siku 21 za maombolezo zilizotolewa, zitakuwa zimemalizika.

## Simba Namtumbo wakarabati ofisi

**Na Gideon Mwakanosya, NAMTUMBO**

SIKU chache baada ya kifo cha shabiki wa Simba, Ally Kuntika , mashabiki wenzake wa timu hiyo wameanza maandalizi ya kukarabati ofisi ya tawi lao ili kumuenzi mwanachama mwenzao aliyefariki baada ya straika, Chris Mugalu kukosa penalti, imefahamika.

Akitoa taarifa ya michango ya papo kwa papo katika kikao cha awali kilichofanyika kwenye viwanja vya Ushirika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namtumbo, Katibu wa Tawi, Yahya Runje alisema kiasi cha Sh. 201,000 kilichangwa.

Runje alisema kiasi hicho cha fedha kilichopatikana kitaanza kufanya kazi ya ukarabati wa chumba cha ofisi kilichopo katika nyumba ya Haji Ngangila pamoja na kununua thamani na vitendea kazi vya ofisi hiyo.

Hata hivyo Runje aliwataka mashabiki wa Simba kujitokeza kufanya kazi za kukarabati ofisi hiyo kwa sababu kiasi cha fedha kilichopatikana kitatumika kununua vifaa vya viwandani na kupunguza gharama za kulipa vibarua.

Naye Ibadi Naimu (Chiba), alisema yupo tayari kujitolea mchanga kwa ajili ya kukarabati huo ulioanza na atauwasilisha kwa viongozi wao.

## Polisi, Biashara zaanza mazoezi

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuimarisha vikosi vyake, timu za Polisi Tanzania na Biashara United zinatarajia kuanza mazoezi leo ili kuwa tayari kukabiliana na ushindani wa mechi za mwisho za Ligi Kuu Bara na mashindano ya Kombe la FA.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alisema anajipanga kuwapa mbinu mpya wachezaji wake kwa sababu anatambua wanakwenda kukutana na timu ngumu yeAlisema kifo cha Rais Magufuli kimemsikitisha kwa sababu kimetokea ghafla na kuongeza kiongozi huyo alikuwa mtu ambaye anapenda maendeleo ya nchi na kueleza mambo mazuri aliyoyaacha yatamfanya akumbukwe wakati wote.

Naye Kocha Msaidizi wa Biashara United, Marwa Chamberi alisema amejipanga kuendeleza yaliyoachwa na aliyekuwa Kocha Mkuu, Francis Baraza kwa ajili ya kufikia malengo ya timu yao.

"Ninaendelea na programu aliyoiacha Baraza huku tukiendelea kusubiri Bodi ya Ligi itangaze rasmi tarehe mpya ya kuanza tena Ligi Kuu," alisema kwa kifupi kocha huyo.

Michezo
Ijumaa Machi 26, 2021
Nipashe



NEYMAR KUSAINI MKATABA MPYA PSG HABARI UK 22

# SIMBA YABADILISHA GIA KUIVAA AS VITA

●●● Lengo ni kuwamaliza Wakongomani hao mapema na kukata tiketi ya kucheza...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

ZIKIWA zimebakia siku nane, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema ameshapata mbinu mpya ya kuwakabili AS Vita katika mchezo wa raundi ya nne ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Aprili 3, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo Gomes amesema wapinzani wao AS Vita huwa na kiwango bora zaidi wanapocheza ugenini.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Gomes alisema amefanikiwa kuwaona wapinzani wake katika mechi za hivi karibuni ikiwamo walipowakabili Al Ahly, ametamba amepata 'dawa' ya kuwatuliza katika mchezo utakaowakutanisha.

Gomes alisema ameona tofauti kubwa katika mechi yao dhidi ya Al Ahly na hiyo ilimpa darasa la kubadilisha mfumo ambao atautumia siku watakapokutana.

Alisema AS Vita walicheza soka la ushindani na walionyesha mabadiliko makubwa kwa kucheza kimbinu tofauti na walipokutana nao jijini Kinshasa katika mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi.

"Nimeona walivyoimarika, nimelifanyia kazi ili kuhakikisha AS Vita hawaondoki na pointi katika mchezo ujao. Tunatambua utakuwa mchezo wenye ushindani mkubwa kwa sababu AS Vita hawatahitaji kufungwa mara mbili, watakuja na mbinu za kutaka kutafuta matokeo chanya, na sisi tunahitaji kutumia uwanja wa nyumbani vizuri,".

"Huu ni mchezo muhimu sana kwetu na imani kubwa wachezaji wangu watapambana ili kupata pointi muhimu kwa ajili ya kujiimarisha na kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hii," alisema Gomes.

Aliongeza anaendelea kuwahimiza wachezaji wake umuhimu wa kushinda mechi hiyo na kukamilisha kazi yao waliyoianza vyema badala ya kusubiri mchezo wa mwisho ambao pia hautakuwa mwepesi kwao.

"Kila mchezaji anajua majukumu ya kufanya uwanjani, nina imani na uwezo wa wachezaji wangu na kutegemea katika kusaka ushindi katika mchezo huo," alisema kocha huyo.

Naye Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, alisema klabu yake imejipanga imara katika kila idara kuhakikisha wanasonga mbele katika michuano hiyo pamoja na kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Mangungu alisema wachezaji wote waliobakia hapa nchini wanaendelea vyema na mazoezi na wanajua 'kiu' ya mafanikio ambayo mashabiki na wanachama wa Simba wanatamani kuifikia msimu huu.

"Nimezungumza na kocha wetu, amesema wachezaji wote ambao wamebaki wanaendelea vizuri na mazoezi na kila mmoja anashauku ya kufanya vizuri katika mchezo huo ambao tunaamini utakuwa na ushindani mkubwa,"alisema Mangungu.

Aliongeza Simba inaendelea kujiimarisha na inawataka mashabiki wake kuachana na maneno ya kuwakatisha tamaa yanayozungumzwa na watu wasioitakia mema timu hiyo.

"Tumesikia maneno mengi ambayo yanasemwa na baadhi ya watu wasioitakia mema timu yetu kwa lengo la kutuvurugia ili tuharibu mipango yetu, tunawaambia tumejidhatiti vizuri, hatuwapi nafasi ya kuturudisha nyuma,"alisema kiongozi huyo.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa Februari 12, mwaka huu mjini Kinshasa, Simba ilipata ushindi wa bao 1-0 huku mchezo wake wa mwisho dhidi ya Al Merreikh walishinda magoli 3-0.



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Rwanda (Amavubi), Meddie Kagere (katikati), akimiliki mpira katika mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), dhidi ya Msumbuji iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamirambo jijini Kigali juzi. Amavubi ilishinda 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## YANGA YAFUNGUKA UBINGWA WANUKIA

**Na Saada Akida**

KUREJEA uwanjani kwa mshabuliaji wa Yanga, Saidi Ntibanzokiza `Saido`, ni taarifa njema kwa mashabiki na wadau wa timu hiyo ambayo imedhamiria kurejesha ufalme wake kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA msimu huu.

Ntibanzokiza alikuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu kwa sababu ya kuwa majeruhi, lakini taarifa rasmi kutoka kwenye kambi ya Timu ya Taifa ya Burundi zinasema afya ya nyota huyo imeimarika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mwambusi alisema amefurahi taarifa za Ntibanzokiza kurejea kikosini na kueleza uwepo wake utaongeza nguvu kwenye timu yake.

Mwambusi alisema anaamini nyota huyo anaendelea kujifua na baada ya kumaliza majukumu ya kimataifa, ataungana na wenzake ili kumalizia mechi za msimu huu zilizobakia.

**"Kuna upungufu nimeuona kwa sasa lakini sitaweza kuweka wazi kwa sababu ya kutokamilika kwa kikosi changu, nina imani ndani ya wiki hii wataporejea wote, hapo tutaangalia kuimarisha safu ya ushambuliaji na sehemu nyingine," alisema Mwambusi.**

Alimtaja mchezaji huyo alikuwa nguzo muhimu kwenye safu ya ushambuliaji, hivyo wanatarajia makali waliyoanza nayo kwenye mzunguko wa pili yatarejea.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002